BENKI KUU YA TANZANIA




# Tathimini Ya Uchumi Ya Mwezi

Agosti 2025

# Yaliyomo

1.0 Mwenendo wa Uchumi wa Dunia....1
2.0 Mwenendo wa Uchumi wa Taifa....3
2.1 Mfumuko wa Bei....3
2.2 Sera ya Fedha....5
2.3 Viwango vya Riba....7
2.4 Masoko ya Fedha....7
2.5 Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali....8
2.6 Mwenendo wa Deni la Taifa....9
2.7 Mwenendo wa Sekta ya Nje....11
3.0 Mwenendo wa Uchumi wa Zanzibar....13
3.1 Mfumuko wa Bei....13
3.2 Shughuli za Bajeti ya Serikali....14
3.3 Mwenendo wa Sekta ya Nje....14
Viambatisho....17

# 1.0 Mwenendo wa Uchumi wa Dunia

Uchumi wa dunia umeendelea kuwa thabiti ukichangiwa na kuboreshwa kwa mazingira ya kifedha pamoja na kupungua kwa athari za ongezeko la ushuru wa bidhaa baina ya mataifa makubwa kibiashara. Pamoja na kuimarika huku, kasi ya ukuaji wa uchumi iko kwenye hatari ya kupungua kutokana na matarajio ya madiliko ya sera za biashara baina ya nchi kubwa kiuchumi duniani (Kielelezo 1.1a na 1.1b).

Kwa ujumla, mfumuko wa bei duniani umeendelea kuwa wa wastani katika maeneo mengi mwezi Julai 2025, ukichangiwa na kupungua kwa vikwazo vya ugavi wa bidhaa na utulivu wa bei za bidhaa muhimu (Kielelezo 1.2). Kutokana na hali hii, benki kuu katika nchi nyingi ziliamua kutobadilisha viwango vya riba ya benki kuu vilivyopo, kwa lengo la kuleta uwiano baina ya kudhibiti matarajio ya mfumuko wa bei katika kipindi cha muda wa kati na kuchochea kasi ya ukuaji wa shughuli za uchumi. Katika ukanda wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika, mfumuko wa bei ulikua na muelekeo wa kupanda kwa baadhi ya nchi na kupungua kwa nchi nyingine, huku katika ukanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, mfumuko wa bei uliendelea kuwa ndani ya kiwango kinachokubalika kwenye mtangamano wa kikanda wa chini ya asilimia 8 (Kielelezo 1.3 na 1.4).

**Kielelezo 1.1a: Fahirisi ya Kutokuwa na-Uhakika ya Sera za Dunia**




Chanzo: https://www.policyuncertainity.com/trade

**Kielelezo 1.1b: Fahirisi ya Kutokuwa-na-Uhakika wa biashara Duniani**




Chanzo : https://worlduncertainityindex.com/

Mwezi Julai 2025, mwenendo wa bei katika soko la bidhaa duniani ulionesha hali isiyotabirika ikilinganishwa na mwezi uliotangulia. Bei ya mafuta ghafi iliendelea kuwa tulivu katika kiwango cha dola za Marekani 69.2 kwa pipa, licha ya nchi za Urusi na Iran kuwekewa vikwazo vipya vya kiuchumi (Jedwali A8). Utulivu huu ulichangiwa kwa kiwango kikubwa na kuongezeka kwa akiba ya mafuta nchini Marekani na China, pamoja na ongezeko la uzalishaji kutoka nchi zisizo wanachama wa OPEC+ ambalo lilifidia upungufu wa uzalishaji kutoka kwa wanachama wa OPEC+. Bei ya dhahabu ilishuka kufuatia kulegezwa kwa vikwazo vya kibiashara duniani. Hali hii ilipelekea kupungua kwa uhitaji wa dhahabu kama sehemu salama ya uwekezaji.

Bei ya kahawa ilishuka zaidi kutokana na msimu wa mavuno unaoendelea nchini Brazil na Vietnam. Bei ya ngano pia ilipungua kutokana na msimu mpya wa mavuno katika nchi za Kaskazini mwa Dunia. Bei ya mahindi na mchele zilipungua ikilinganishwa na mwezi uliopita, kutokana na wingi wa usambazaji wa bidhaa za mauzo ya nje na kupungua kwa mahitaji ya uagizaji. Wakati huohuo, bei ya sukari ilishuka kidogo kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji katika nchi zinazoongoza kwa uzalishaji wa bidhaa hiyo, hususan Brazil, India na Thailand. Kwa upande mwingine, bei ya tumbaku ilipanda kutokana na ongezeko la mahitaji duniani, hususan katika ukanda wa Asia-Pacific. Bei ya mafuta ya mawese pia iliongezeka, ikichochewa na mahitaji makubwa na kuimarika kwa ushindani. Bei ya mbolea iliendelea kupanda, ikionyesha ongezeko la mahitaji maeneo

mengi duniani (Kielelezo 1.5).

**Kielelezo 1.2: Mfumuko wa Bei kwa Nchi Zinazoendelea na Zinazochipukia Kiuchumi**




Chanzo: Bloomberg

**Kielelezo 1.3: Mfumuko wa Bei Miongoni mwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki**




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu
Tanbihi: Mistari ya nukta inaashiria viwango vya mfumuko wa bei vilivyokusudiwa (inflation target)

**Kielelezo 1.4: Mfumuko wa Bei Miongoni mwa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika**




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu
Tanbihi: Mistari ya nukta inaashiria viwango vya mfumuko wa bei vilivyokusudiwa (inflation target)

**Kielelezo 1.5: Bei za Bidhaa katika Soko la Dunia**




Chanzo: http://www.worldbank.org/prospects
Tanbihi: DAP Inaashiria Di-ammonium phosphate

# 2.0 Mwenendo wa Uchumi wa Taifa

## 2.1 Mfumuko wa Bei

Kiwango cha mfumuko wa bei kimeendelea kuwa ndani ya wigo wa lengo la nchi na vigezo vya mtangamano wa kiuchumi kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (Kielelezo 2.1.1). Kwa mwezi wa

Julai 2025, mfumuko wa bei ulikua kwa asilimia 3.3, sawasawa na mfumuko wa bei katika mwezi wa Juni 2025. Matokeo haya yanaakisi ongezeko la mfumuko wa bei wa vyakula na vinywaji baridi lililofidiwa na kupungua kwa kasi ya mfumuko wa bei kupungua kwa bei za bidhaa za msingi kama mafuta, umeme na nishati (Jedwali 2.1.1).

### Jedwali 2.1.1: Maendeleo ya Mfumuko wa Bei

2020 = 100

| Makundi Makuu ya Fahirisi | Mizania | Badiliko la Mfumuko wa bei (Asilimia) | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Badiliko: Mwezi hadi Mwezi | | | Badiliko kwa Mwaka | | |
| | | Julai-24 | Juni-25 | Julai-25 | Julai-24 | Juni-25 | Julai-25 |
| Vyakula na vinywaji baridi | 28.2 | -1.1 | 0.7 | -0.8 | 0.9 | 7.3 | 7.6 |
| Vinywaji vikali na tumbaku | 1.9 | 0.6 | 0.1 | 0.1 | 3.2 | 3.5 | 3.0 |
| Nguo, mavazi na viatu | 10.8 | 0.1 | 0.2 | 0.0 | 1.8 | 2.0 | 1.9 |
| Makazi, maji, umeme, gesi na nishati zinginezo | 15.1 | -0.1 | 0.2 | -0.4 | 6.6 | 1.7 | 1.3 |
| Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa makazi | 7.9 | 0.3 | 0.0 | 0.6 | 3.5 | 2.0 | 2.4 |
| Afya | 2.5 | 0.3 | 0.0 | 0.1 | 1.9 | 1.8 | 1.6 |
| Usafiri | 14.1 | 0.3 | 0.0 | 0.0 | 5.2 | 1.6 | 1.2 |
| Habari na mawasiliano | 5.4 | -0.1 | 0.0 | 0.0 | 1.7 | 0.0 | 0.2 |
| Burudani, michezo na utamaduni | 1.6 | 0.3 | -0.1 | -0.1 | 3.3 | 1.4 | 1.0 |
| Elimu | 2.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 3.4 | 3.1 | 3.1 |
| Migahawa na huduma za malazi | 6.6 | 0.3 | 0.0 | 0.0 | 2.8 | 1.3 | 1.0 |
| Bima na huduma za kifedha | 2.1 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 1.7 | 0.6 | 0.6 |
| Huduma binafsi, hifadhi ya jamii na bidha na huduma mchanganyiko | 2.1 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 7.2 | 2.0 | 2.0 |
| Bidhaa zote | 100.0 | -0.2 | 0.3 | -0.3 | 3.1 | 3.3 | 3.3 |
| Makundi mengine teule | | | | | | | |
| Bidhaa za msingi | 73.9 | 0.2 | 0.2 | 0.0 | 3.6 | 2.1 | 1.9 |
| Fahirisi isiyojumuisha fahirishi za bidhaa za msingi | 26.1 | -0.4 | -0.2 | 1.0 | 1.8 | 5.6 | 7.1 |
| Mafuta, nishati na bili za maji | 5.7 | 4.1 | 0.0 | 0.2 | 13.5 | 6.1 | 2.1 |
| Huduma | 37.2 | 0.2 | 0.0 | 0.0 | 2.9 | 1.0 | 0.9 |
| Bidhaa | 62.8 | 0.0 | 0.1 | 0.4 | 3.2 | 4.2 | 4.7 |
| Bidhaa na huduma za elimu | 4.1 | 0.3 | 0.0 | 0.0 | 3.7 | 3.2 | 2.9 |
| Bidhaa zote isipokuwa chakula na vinywaji visivyo na kilevi | 71.8 | 0.5 | 0.1 | 0.1 | 4.0 | 2.1 | 1.7 |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Uchanganuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

### Kielelezo 2.1.1: Mfumuko wa Bei na Malengo Yake

Asilimia




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Uchanganuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

Mfumuko wa bei za vyakula na vinywaji baridi ulikua kwa asilimia 7.6 katika mwezi Julai 2025, kutoka asilimia 7.3 ya mwezi Juni 2025 na asilimia 1.0 mwezi Julai 2024. Ongezeko la mfumuko wa bei limechangiwa na ongezeko la bei za vyakula vya nafaka, kama mchele, mtama na uwele (Kielelezo 2.1.2a and Kielelezo 2.1.2b).

Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) ilitoa jumla ya tani 1,855.3 za mahindi mwezi Julai 2025. Pamoja na kiwango hiki kutolewa, NFRA iliendelea kuwa na akiba ya tani 485,930.4, ambayo ni kubwa ikilinganishwa na tani 368,855 kwenye kipindi kama hicho mwaka 2024. Hali hii ilichangiwa na mavuno mazuri katika msimu uliopita wa kilimo pamoja na upatikanaji wa fedha za kutosha kwa ajili ya ununuzi wa mazao (Jedwali 2.1.2)

### Kielelezo 2.1.2: Kiwango cha Mfumuko wa Bei za Mazao

#### a. Mazao ya vyakula vikuu

Asilimia




Chanzo: Wizara ya Viwanda na Biashara, na Uchanganuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

#### b. Mazao ya vyakula mbadala

Asilimia




Chanzo: Wizara ya Viwanda na Biashara, na Uchanganuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

**Jedwali 2.1.2: Akiba ya Chakula katika Hifadhi ya Chakula**

Tani

| Kipindi | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Jan | 43,597 | 110,398 | 207,899 | 124,736 | 270,984 | 646,480 |
| Feb | 41,231 | 110,389 | 203,297 | 106,881 | 326,172 | 619,659 |
| Mac | 39,597 | 109,231 | 200,626 | 80,123 | 336,099 | 587,062 |
| Apr | 38,053 | 109,231 | 190,366 | 63,808 | 340,102 | 557,228 |
| Mei | 38,291 | 108,284 | 149,402 | 51,367 | 340,002 | 509,990 |
| Jun | 52,725 | 107,384 | 141,576 | 46,665 | 340,479 | 477,923 |
| Jul | 90,255 | 107,384 | 140,695 | 94,088 | 368,855 | 485,930 |
| Ago | 92,991 | 123,635 | 144,410 | 210,020 | 489,187 | |
| Sep | 109,733 | 150,057 | 149,044 | 244,169 | 651,403 | |
| Okt | 110,895 | 192,408 | 151,794 | 244,289 | 708,399 | |
| Nov | 110,289 | 209,057 | 147,401 | 244,223 | 702,502 | |
| Des | 110,398 | 214,968 | 137,655 | 248,282 | 677,115 | |

Chanzo: Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula.

Mfumuko wa bei za bidhaa za msingi (core inflation) ulikua kwa asilimia 1.9 katika mwezi Julai 2025, sawa na mwezi Juni 2025, ukishuka kutoka asilimia 3.6 mwezi Julai 2024. Usawa kati ya mwezi Agosti na Julai 2025 unaakisi utulivu wa bei za malazi na huduma (Kielelezo 2.1.3). Hali hii imechangiwa pia na kupungua kwa bei za bidhaa katika masoko ya kimataifa. Kwa upande wa mchango, kundi la vyakula visivyochakatwa limeendelea kuchangia zaidi katika mfumuko wa bei, ikifuatiwa na bidhaa za msingi na nishati (Kielelezo 2.1.4).

**Kielelezo 2.1.3: Viwango vya Mfumuko wa Bei kwa Miezi Kumi na Mbili**

Asilimia




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Uchanganuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

**Kielelezo 2.1.4: Mchango katika Mfumuko wa Bei**

Asilimia




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Uchanganuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

Mfumuko wa bei za nishati, mafuta na huduma za msingi ulishuka hadi asilimia 1.0 kwa mwezi Julai 2025, kutoka asilimia 2.1 mwezi Juni 2025 na asilimia 1.5 mwezi Julai 2024 (Kielelezo 2.1.3). Kupungua huku kulitokana na kushuka zaidi kwa bei za mkaa. Aidha, bei za bidhaa zitokanazo na mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa katika mwezi husika ziliendelea kushuka, sambamba na mwenendo wa soko la dunia (Kielelezo 2.1.5). Kupungua huku kumechangia kuleta ustahimilivu wa mfumuko wa bei wa jumla.

**Kielelezo 2.1.5: Bei za Ndani za Mafuta ya Petroli, Diseli na Mafuta ya Taa**

Shilingi kwa lita




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

## 2.2 Sera ya Fedha

Kamati ya Sera ya Fedha, katika kikao chake cha 237 kilichofanyika mwezi wa Julai 2025, iliamua kupunguza Riba ya Benki Kuu (CBR) kutoka asilimia 6.00 hadi asilimia 5.75 kwa robo mwaka inayoishia Septemba 2025. Uamuzi huu ulichukuliwa kwa lengo la kuongeza ukuaji wa mikopo kwenye sekta ya binafsi ili kuchochea zaidi shughuli za kiuchumi. Uamuzi huu pia ulizingatia mwelekeo wa mfumuko wa bei ambao unatarajiwa kuendelea kuwa chini ya asilimia 5; vihatarishi vinavyotokana na kutotabirika kwa mwenendo wa uchumi wa dunia, na kuendelea kuimarika kwa hali ya uchumi wa ndani. Kwa muktadha huu, Benki Kuu imeendelea kutekeleza sera ya fedha kwa lengo la kuhakikisha kuwa riba ya mikopo ya siku 7 katika soko la fedha baina ya benki inakuwa ndani ya wigo wa asilimia 3.75 hadi asilimia 7.75.

Katika utekelezaji wa Sera ya Fedha, Benki Kuu ilitoa mikopo ya muda mfupi (reverse repo) yenye thamani ya Shilingi bilioni 758.8 mwezi wa Julai 2025, kwa lengo la kuimarisha hali ya ukwasi katika mfumo wa kibenki. Hatua hii ilipelekea riba ya mikopo ya siku saba katika soko la fedha baina ya mabenki kubaki ndani ya wigo wa Riba ya Benki Kuu (Kielelezo 2.2.1 na 2.2.2).

**Kielelezo 2.2.1: Mikopo ya Muda Mfupi kwa Mabenki**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

### Mfumo wa Sera ya Fedha wa Benki Kuu ya Tanzania.

Jukumu la msingi la Benki Kuu ya Tanzania ni kuandaa na kutekeleza sera ya fedha. Sera ya fedha inajumuisha hatua au maamuzi yanayolenga kuthibiti ujazi wa fedha katika uchumi ambao huchangia katika kuamua viwango vya riba vinavyopangwa na benki na taasisi za fedha kwa wateja wao, na hivyo kuathiri mfumuko wa bei na ukuaji wa pato la taifa.

Malengo ya sera ya fedha ni kudumisha utulivu wa bei, ikiwa na maana ya kuwa na kiwango cha chini na tulivu cha mfumuko wa bei kwa muda mrefu, pamoja na kusaidia ukuaji wa uchumi. Mfumuko wa bei hupimwa kwa mabadiliko ya mwaka ya fahirisi ya bei za mlaji (Consumer Price Index), ambayo huwasilishwa kwa asilimia. Kwa kipindi cha kati (hadi miaka 5), lengo la mfumuko wa bei ni kuwa kati ya asilimia 3 hadi 5.

Ili kutekeleza malengo haya, Kamati ya Sera ya Fedha hufanya tathmini ya hali ya uchumi na kuamua kiwango cha riba ya Benki Kuu (Central Bank Rate kwa lengo la kuthibiti mfumuko wa bei na kukuza uchumi. Benki Kuu ya Tanzania hutekeleza sera ya fedha kwa kuhakikisha kuwa kiwango cha riba ya mikopo ya siku 7 baina ya benki, ambayo ni kipimo cha utekelezaji kinachoendana na Riba ya Benki Kuu.

Benki Kuu ya Tanzania hutumia nyenzo mbalimbali za sera ya fedha ili kuhakikisha kuwa lengo la uendeshaji linaendana na riba ya Benki Kuu. Nyenzo kuu za utekelezaji wa Sera ya fedha ni pamoja na mikopo ya muda mfupi baina ya Benki Kuu na benki za biashara (repo and reverse repo), dhamana za Serikali za siku 35 na 91, kiwango cha amana za benki za biashara kinachotakiwa kuwekwa kisheria Benki Kuu (*Statutory Minimum Reserve* Requirement *Ratio*) na uuzaji na ununuzi wa fedha za kigeni baina ya benki katika soko la jumla la fedha za kigeni. Pamoja na nyenzo hizo, Benki Kuu pia hutoa mikopo ya muda mfupi ambayo hutakiwa kurudishwa ndani ya siku husika na ile ya siku moja (*Intraday and Lombard loan facilities*) ili kusaidia uwepo wa ufanisi katika mifumo ya malipo na ufanyaji wa miamala.

Benki Kuu ya Tanzania hutekeleza jukumu lake la kuandaa na kutekeleza wa sera ya fedha kwa uwazi. Maamuzi ya Kamati ya Sera ya Fedha, ikiwemo kuhusu riba ya Benki Kuu huwasilishwa kwenye mikutano ya Gavana na wakuu wa taasisi za kibenki na pia kwa umma kupitia vyombo vya habari. Vilevile, Benki Kuu huchapisha Tamko la Kamati ya Sera ya Fedha na taarifa mbalimbali zinazoainisha mwelekeo wa sera ya fedha, matokeo ya utekelezaji wake na mwenendo wa uchumi kwa ujumla. Taarifa hizi zinapatikana kupitia tovuti ya Benki Kuu ya Tanzania (www.bot.go.tz ).

### Kielelezo 2.2.2: Riba ya Benki Kuu na Riba ya Mikopo ya Siku 7




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na mabenki

Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikua kwa asilimia 19.9 mwaka ulioishia Julai 2025, ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 18.7 mwezi uliotangulia, sambamba na mwelekeo wa sera ya fedha (Kielelezo 2.2.3 na Jedwali 2.2.1). Ukuaji huu ulitokana na ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi (Kielelezo 2.2.4). Mikopo kwa sekta binafsi iliendelea kukua kwa kasi, ikiongezeka kwa asilimia 15.9, sawa na kiwango kilichorekodiwa mwezi uliotangulia (Kielelezo 2.2.5).

### Kielelezo 2.2.3:Mwenendo wa Ujazi wa Fedha




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na mabenki

### Jedwali 2.2.1: Ujazi wa Fedha na Vipengele Vyake

| | Kiasi (Shilingi Billioni) | | | Ukuaji kwa mwaka (%) | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Jul-24 | Jun-25 | Jul-25 | Jul-24 | Jun-25 | Jul-25 |
| Rasilimali halisi za nje | 12,226.7 | 15,509.5 | 15,726.1 | 13.5 | 26.7 | 28.6 |
| Rasilimali halisi za nje za Benki Kuu | 12,227.6 | 13,623.0 | 13,884.0 | 7.4 | 10.3 | 13.5 |
| Rasilimali halisi za nje za mabenki | -0.9 | 1,886.5 | 1,842.1 | --- | --- | --- |
| Rasilimali halisi za ndani | 34,704.7 | 39,973.8 | 40,565.0 | 8.9 | 15.8 | 16.9 |
| Madai rasmi ya ndani | 47,250.2 | 52,610.3 | 52,147.8 | 13.9 | 13.2 | 10.4 |
| Amana za Serikali zilizopo Benki Kuu na Benki za Biashara | 8,467.3 | 7,988.1 | 7,961.4 | -5.7 | -7.3 | -6.0 |
| Mikopo kwa sekta binafsi | 35,354.6 | 40,549.0 | 40,972.2 | 17.6 | 15.9 | 15.9 |
| Rasilimali nyinginezo | -12,545.5 | -12,636.5 | -11,582.8 | 30.7 | 5.9 | -7.7 |
| Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) | 46,931.4 | 55,483.3 | 56,291.1 | 10.1 | 18.7 | 19.9 |
| Amana za fedha za kigeni | 11,450.8 | 13,769.3 | 13,653.2 | 16.5 | 19.8 | 19.2 |
| Ujazi wa fedha, kwa tafsiri pana (M2) | 35,480.6 | 41,714.0 | 42,637.9 | 8.1 | 18.3 | 20.2 |
| Amana zinginezo | 13,304.6 | 16,060.1 | 16,406.3 | 8.1 | 21.0 | 23.3 |
| Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1) | 22,176.0 | 25,653.9 | 26,231.6 | 8.1 | 16.6 | 18.3 |
| Ujazi wa fedha ulio kwenye mzunguko | 7,085.6 | 7,874.8 | 8,122.1 | 11.6 | 11.3 | 14.6 |
| Amana za hundi | 15,090.3 | 17,779.1 | 18,109.4 | 6.6 | 19.2 | 20.0 |
| Fedha za msingi (M0) | 10,896.5 | 12,451.7 | 13,423.8 | 6.9 | 14.0 | 23.2 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania, mabenki
Tanbihi: "---" Inaashiria ukuaji unaozidi asilimia 100

### Kielelezo 2.2.4: Mchango katika Ukuaji wa M3




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania, mabenki

### Kielelezo 2.2.5: Mwenendo wa Mikopo kwa Sekta Binafsi




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na mabenki

Ukuaji wa mikopo inayoelekezwa kwenye shughuli za kilimo umeendelea kuimarika, ambapo mwezi Julai 2025, ukuaji ulifikia asilimia 31.8, zikifuatiwa na shughuli za uchimbaji madini na mawe, kwa asilimia 26.2, na uchukuzi na mawasiliano, kwa asilimia 21.6 (Jedwali 2.2.2). Wakati huohuo, mikopo kwa shughuli binafsi, ambayo hutumika kugharamia biashara ndogo na za kati iliendelea kuchukua sehemu kubwa ya mikopo yote, kwa asilimia 35.5, ikifuatiwa na biashara na kilimo zilizokuwa na asilima 14 na asilimia 13.3, mtawalia (Kielelezo 2.2.6)

### Jedwali 2.2.2: Ukuaji wa Mikopo kwa Shughuli za Uchumi

Asilimia

| | Jul-24 | Des-24 | Jan-25 | Feb-25 | Mac-25 | Apr-25 | Mei-25 | Jun-25 | Jul-25 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kilimo | 44.6 | 41.0 | 41.6 | 37.2 | 36.3 | 29.8 | 29.8 | 30.2 | 31.8 |
| Ujenzi | 16.3 | 13.2 | 14.8 | 14.5 | 22.4 | 23.8 | 25.6 | 25.7 | 18.9 |
| Uchukuzi na mawasiliano | 11.6 | 11.6 | 19.0 | 23.1 | 35.1 | 39.2 | 27.9 | 25.7 | 21.6 |
| Biashara | 0.3 | 2.7 | 1.3 | 4.6 | 5.4 | 7.0 | 21.7 | 22.5 | 13.0 |
| Uchimbaji Madini | 0.8 | 5.6 | 5.0 | 5.8 | 12.7 | 14.4 | 24.1 | 21.3 | 26.2 |
| Hoteli na migahawa | 19.5 | -36.3 | -30.6 | -28.2 | -24.8 | -10.5 | 22.9 | 20.8 | 0.8 |
| Shughuli binafsi | 17.7 | 14.7 | 13.9 | 13.1 | 9.4 | 14.7 | 13.6 | 13.7 | 13.1 |
| Viwanda | 23.9 | 16.3 | 18.0 | 16.9 | 10.9 | 7.7 | 7.3 | 2.5 | 6.3 |

Chanzo: Mabenki na Uchanganuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

**Kielelezo 2.2.6: Mchango wa Shughuli za Kiuchumi katika Ukuaji wa Mikopo**

Asilimia




Chanzo: Mabenki na Uchanganuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

## 2.3 Viwango vya Riba

Mwenendo wa riba za mikopo na amana za mabenki hazikuonyesha mabadiliko makubwa katika kipindi cha mwezi Julai 2025, ikilinganishwa na mwezi uliotangulia. Wastani wa riba za mikopo ulipungua kwa kasi ndogo hadi kufikia asilimia 15.16, kutoka asilimia 15.23 mwezi uliotangulia (Jedwali 2.3.1). Vilevile, riba za mikopo ya wateja wakubwa (negotiated lending rates) zilipungua kidogo kutoka asilimia 12.68 hadi asilimia 12.56. Riba za amana ziliongezeka kwa kasi ndogo hadi wastani wa asilimia 8.83, kutoka asilimia 8.74. Aidha, riba za amana za wateja wakubwa (negotiated deposit rate) zilipungua hadi asilimia 10.72 kutoka asilimia 11.21 iliyorekodiwa mwezi uliotangulia. Wigo kati ya riba za mikopo na amana za mwaka ulipungua hadi asilimia 5.63, kutoka asilimia 6.66 mwezi Julai 2024.

**Jedwali 2.3.1: Riba za Amana na Mikopo Inayotolewa na Benki za Biashara**

Asilimia

| | Jul-24 | Des-24 | Jan-25 | Feb-25 | Mac-25 | Apr-25 | Mei-25 | Jun-25 | Jul-25 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Riba za amana | 2.87 | 2.84 | 2.97 | 2.98 | 2.86 | 2.89 | 2.52 | 2.90 | 2.90 |
| Riba ya mikopo - jumla | 15.29 | 15.71 | 15.73 | 15.14 | 15.50 | 15.16 | 15.18 | 15.23 | 15.16 |
| Riba za mikopo (mwaka 1) | 15.67 | 15.74 | 15.70 | 15.77 | 15.83 | 16.15 | 15.96 | 15.69 | 15.51 |
| Riba za mikopo (wateja wakubwa) | 12.78 | 12.83 | 12.80 | 13.42 | 12.94 | 12.88 | 12.99 | 12.68 | 12.56 |
| Riba za amana -jumla | 8.15 | 8.33 | 8.31 | 8.13 | 8.00 | 7.82 | 8.58 | 8.74 | 8.83 |
| Riba za amana (miezi 12) | 9.01 | 9.62 | 10.08 | 9.48 | 8.14 | 9.27 | 9.72 | 9.79 | 9.88 |
| Riba za amana (wateja wakubwa) | 9.96 | 10.39 | 11.80 | 11.40 | 10.35 | 10.52 | 10.64 | 11.21 | 10.72 |
| Tofauti kati ya riba za mikopo na amana | 6.66 | 6.12 | 5.63 | 6.29 | 7.69 | 6.88 | 6.24 | 5.90 | 5.63 |

Chanzo: Mabenki na Uchanganuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

## 2.4 Masoko ya Fedha

### Soko la Dhamana za Serikali

Benki Kuu iliendesha minada miwili ya dhamana za Serikali zenye thamani ya Shilingi bilioni 162. Kiasi kikubwa cha dhamana hizo kilikuwa kwa ajili ya kugharamia matumizi ya Serikali, na kiwango kilichosalia kwa ajili ya kusaidia ufanisi wa soko la fedha nchini. Minada hii ilipokea zabuni zaidi ya thamani iliotangazwa, na kufikia jumla ya shilingi bilioni 452.1, hali ilioakisi uwepo wa ukwasi wa kutosha katika uchumi. Aidha, shilingi bilioni 158.9 zilikubaliwa. Kufuatia mwendendo huu, riba za dhamana za Serikali zilipungua hadi wastani wa asilimia 8.13 kutoka asilimia 8.89 iliyorekodiwa mwezi uliopita.

**Kielelezo 2.4.1: Mwenendo wa Minada ya Dhamana za Serikali**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Vilevile, Benki Kuu iliendesha minada ya hatifungani za miaka 2, 5, na 10 yenye thamani ya Shilingi bilioni 117.05, bilioni 136.2 na bilioni 162.8, mtawalia. Minada ya miaka 2 na miaka 5 ilikuwa na mahitaji madogo, huku ule wa miaka 10 ulikuwa na mahitaji makubwa kutokana na wawekezaji wengi kupendelea zaidi hati fungani za muda mrefu. Kwa ujumla, minada ilipokea zabuni zenye thamani ya shilingi bilioni 396.4, ambapo zabuni zenye thamani ya shilingi bilioni 351.9 zilikubaliwa. Riba za hati fungani za miaka 2 na 5 ziliongezeka hadi asilimia 12.17 na asilimia 13.18, mtawalia, wakati riba ya hati fungani ya miaka 10 ilipungua kidogo hadi asilimia 13.74.

### Soko la Fedha Baina ya Mabenki

Soko la fedha baina ya mabenki (IBCM) liliendelea kutumika kufanya mauziano ya kutunisha ukwasi wa shilingi kati ya mabenki na hivyo kuchangia utekelezaji na ufanisi wa sera ya fedha. Thamani ya mauzo katika soko ilifikia shilingi bilioni 3,746 mwezi Julai 2025, ikilinganishwa na shilingi bilioni 2,873.9 mwezi Juni 2025 (Kielelezo 2.4.2). Mauziano ya siku saba yalishika nafasi kubwa, yakiwa na asilimia 65.9. Riba ya jumla ya soko ilipungua hadi asilimia 6.62 kutoka asilimia 7.93 Juni 2025.

**Kielelezo 2.4.2: Mwenendo wa Soko la Fedha Baina ya Mabenki**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

### Soko la Fedha za Kigeni

Hali ya ukwasi katika Soko la Fedha za Kigeni baina ya Mabenki (IFEM) iliendelea kuimarika mwezi Julai 2025, ikichochewa na mapato ya mauzo ya mazao ya biashara na dhahabu nje ya nchi. Kufuatia mwenendo huu, mauzo ya fedha za kigeni katika soko yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 162.5, kutoka dola za Marekani milioni 121.5 mwezi Juni 2025. Wakati huohuo, Benki Kuu ilishiriki katika soko kwa kuzingatia Sera ya Ushiriki katika soko la fedha za nigeni kwa kuuza dola za Marekani milioni 17.5 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 6.3 kwa mwezi uliotangulia (Kielelezo 2.4.3).

Shilingi iliendelea kuwa thabiti, ikibadilishwa kwa wastani wa Shilingi 2,666.79 kwa dola moja ya Marekani mwezi Julai 2025, ikilinganishwa na Shilingi 2,631.56 kwa dola moja ya Marekani mwezi uliopita. Hii ni sawa na kushuka kwa thamani ya Shilingi kwa asilimia 0.11 kwa mwaka ulioishia Julai 2025, ikilinganishwa na asilimia 0.21 mwaka ulioishia Juni 2025.

**Kielelezo 2.4.3: Mwenendo wa Soko la Fedha za Kigeni**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## 2.5 Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali

Mwezi Juni 2025, makusanyo ya mapato ya Serikali yalivuka lengo la mwezi kwa asilimia 5.1, ambapo jumla ya mapato yalifikia shilingi bilioni 3,753.4. Kati ya kiasi hicho, Serikali Kuu ilikusanya shilingi bilioni 3,679.2, sawa na asilimia 95.4 ya mapato yote ya ndani, na kuzidi lengo la mwezi la shilingi bilioni 3,444.3.

Mwenendo wa mapato ya kodi uliendelea kuwa mzuri, ambapo mapato ya kodi yalifikia shilingi bilioni 3,108.7, yakivuka lengo la mwezi kwa asilimia 7.8. Mafanikio haya ni matokeo ya juhudi zinazoendelea kuboresha ukusanyaji na usimamizi wa kodi. Pamoja na mafanikio haya, mapato yasiyo ya kodi yalifikia shilingi bilioni 470.5, chini ya lengo la mwezi la kukusanya shilingi bilioni 561.5 (Kielelezo 2.5.1).

**Kielelezo 2.5.1: Mapato ya Serikali Kuu Mwezi Juni 2025**

Shilingi bilioni




Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: Takwimu halisi za mwaka 2025 ni za awali

Mwezi Juni, 2025 Serikali iliendelea kuwianisha matumizi yake na vyanzo mbalimbali za fedha. Jumla ya matumizi ya Serikali katika mwezi June 2025 yalifikia shilingi bilioni 3,350.0, ambapo shilingi bilioni 2,440.6 zilitumika kwa matumizi ya kawaida, huku shilingi bilioni 909.4 zilielekezwa kwenye miradi ya maendeleo (Kielelezo 2.5.2).

**Kielelezo 2.5.2: Matumizi ya Serikali Kuu Mwezi Juni 2025**

Shilingi bilioni




Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: Takwimu halisi za mwaka 2025 ni za awali

## 2.6 Mwenendo wa Deni la Taifa

Deni la Taifa lilifikia dola za Marekani milioni 46,586.6 mwishoni wa mwezi Juni 2025, sawa na ongezeko la asilimia 1.0 ikilinganishwa na kiwango kilichorekodiwa mwishoni mwa Mei 2025. Kati ya kiasi hicho, asilimia 70.7 ilikuwa ni deni la nje.

### Deni la Nje

Deni la Taifa (linalojumuisha deni la Serikali la ndani na la nje, na deni la nje la sekta binafsi) liliongezeka kwa asilimia 0.1 mwezi Juni 2025, na kufikia dola za Marekani milioni 32,955.5 mwishoni mwa mwezi huo. Katika kiasi hicho, asilimia 85.4 ilikuwa deni la nje la Serikali, huku sehemu iliyobaki ikiwa deni la nje la sekta binafsi (Jedwali 2.6.1).

Mikopo ya nje iliyopokelewa mwezi Juni 2025 ilikuwa dola za Marekani milioni 868.4, ambapo sehemu kubwa ilipokelewa na Serikali Kuu. Aidha, kiasi cha dola za Marekani milioni 234.4 kilitumika kulipia deni la nje, ambapo dola za Marekani milioni 173.6 zilitumika kulipa marejesho ya mkopo mkuu na kiasi kilichobaki malipo ya riba.

Mchanganuo wa deni la nje kwa aina ya wakopeshaji ulikuwa sawa na mwezi uliotangulia na kipindi kama hicho cha mwaka 2024. Mashirika ya kifedha ya kimataifa yaliendelea kuwa wadai wakuu wa Serikali, yakifuatiwa na wakopeshaji wa kibiashara (Jedwali 2.6.2). Aidha, sekta za usafirishaji na mawasiliano zilibaki kuwa wanufaika wakubwa wa mikopo ya nje. Dola ya Marekani iliendelea kuwa sarafu kuu ya deni la nje, ikifuatiwa na sarafu ya Umoja wa Ulaya, Euro (Jedwali 2.6.3 na 2.6.4).

**Jedwali 2.6.1: Mchanganuo wa Deni la Nje kwa Kundi la Wakopaji**

Dola za Marekani Milioni

| | Jun-24 | | Mei-25[r] | | Jun-25[p] | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mkopaji | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) |
| Serikali Kuu | 24,569.4 | 76.9 | 27,127.1 | 82.4 | 28,133.7 | 85.4 |
| Deni ambalo halijalipwa | 24,317.5 | 76.1 | 27,048.7 | 82.2 | 28,055.0 | 85.1 |
| Malimbikizo ya riba | 251.9 | 0.8 | 78.4 | 0.2 | 78.7 | 0.2 |
| Sekta binafsi | 7,377.7 | 23.1 | 5,775.4 | 17.6 | 4,820.6 | 14.6 |
| Deni ambalo halijalipwa | 6,094.8 | 19.1 | 5,288.0 | 16.1 | 4,630.7 | 14.1 |
| Malimbikizo ya riba | 1,282.9 | 4.0 | 487.4 | 1.5 | 189.9 | 0.6 |
| Mashirika ya umma | 3.8 | 0.0 | 3.8 | 0.0 | 1.3 | 0.0 |
| Deni ambalo halijalipwa | 3.8 | 0.0 | 3.8 | 0.0 | 1.3 | 0.0 |
| Malimbikizo ya riba | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Jumla ya deni la nje | 31,950.9 | 100.0 | 32,906.2 | 100.0 | 32,955.5 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizorekebishwa; p, takwimu za awali; na TANESCO, ATCL, TRC, TPA, TFC na DAWASA hazina deni la nje ambalo halijalipwa

**Jedwali 2.6.2: Mchanganuo wa Deni la Nje kwa Kundi la Wakopeshaji**

Dola za Marekani Milioni

| | Jun-24 | | Mei-25ʳ | | Jun-25ᵖ | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mkopeshaji | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) |
| Mashirika ya fedha ya kimataifa | 17,148.6 | 53.7 | 18,993.4 | 57.7 | 19,328.5 | 58.7 |
| Deni ambalo halijalipwa | 17,052.9 | 53.4 | 18,960.2 | 57.6 | 19,302.5 | 58.6 |
| Malimbikizo ya riba | 95.6 | 0.3 | 33.2 | 0.1 | 26.0 | 0.1 |
| Washirika wa maendeleo | 1,360.2 | 4.3 | 1,442.5 | 4.4 | 1,525.5 | 4.6 |
| Deni ambalo halijalipwa | 1,108.4 | 3.5 | 1,364.2 | 4.1 | 1,446.8 | 4.4 |
| Malimbikizo ya riba | 251.9 | 0.8 | 78.4 | 0.2 | 78.7 | 0.2 |
| Benki za kimataifa za biashara | 11,742.1 | 36.8 | 11,448.4 | 34.8 | 11,458.3 | 34.8 |
| Deni ambalo halijalipwa | 10,944.2 | 34.3 | 11,161.9 | 33.9 | 11,325.9 | 34.4 |
| Malimbikizo ya riba | 797.9 | 2.5 | 286.4 | 0.9 | 132.5 | 0.4 |
| Mikopo ya mauzo ya nje | 1,700.0 | 5.3 | 1,021.9 | 3.1 | 643.3 | 2.0 |
| Deni ambalo halijalipwa | 1,310.5 | 4.1 | 854.2 | 2.6 | 611.8 | 1.9 |
| Malimbikizo ya riba | 389.5 | 1.2 | 167.8 | 0.5 | 31.5 | 0.1 |
| Jumla ya deni la nje | 31,950.9 | 100.0 | 32,906.2 | 100.0 | 32,955.5 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizorekebishwa; na p, takwimu za awali

**Jedwali 2.6.3: Matumizi ya Deni Lililotolewa na Bado Halijalipwa, kwa Asilimia**

| Shughuli ya uchumi | Jun-24 | Mei-25ʳ | Jun-25ᵖ |
|---|---|---|---|
| Urari wa malipo na msaada wa bajeti | 17.6 | 21.1 | 22.0 |
| Usafirishaji na mawasiliano | 21.3 | 21.9 | 22.1 |
| Kilimo | 5.1 | 5.2 | 5.3 |
| Nishati na madini | 15.2 | 12.6 | 12.7 |
| Viwanda | 4.0 | 2.5 | 2.2 |
| Huduma za jamii na elimu | 20.3 | 20.7 | 20.7 |
| Fedha na bima | 3.9 | 4.3 | 3.6 |
| Utalii | 1.7 | 1.8 | 1.7 |
| Mali isiyohamishika na ujenzi | 5.0 | 4.6 | 4.4 |
| Mengineyo | 5.8 | 5.3 | 5.2 |
| Jumla | 100.0 | 100.0 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha, na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizorekebishwa; p, takwimu za awali.

**Jedwali 2.6.4: Deni Ambalo Halijalipwa Kwa Muundo wa Sarafu, kwa Asilimia**

| Sarafu | Jun-24 | Mei-25ʳ | Jun-25ᵖ |
|---|---|---|---|
| Dola ya Marekani | 67.9 | 66.0 | 65.3 |
| Euro | 16.2 | 17.6 | 17.9 |
| Yuan ya China | 6.2 | 6.3 | 6.6 |
| Nyingine | 9.6 | 10.1 | 10.1 |
| Total | 100.0 | 100.0 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizobadilishwa; na p, takwimu za awali

## Deni la Ndani

Hadi mwisho wa mwezi Julai 2025, deni la ndani la Serikali lilifikia shilingi bilioni 35,351.4, kiasi hicho ni pungufu kwa asilimia 0.4 ukilinganisha na mwezi ulipita (Kielelezo 2.6.1). Deni litokanalo na dhamana za Serikali za muda mrefu liliendelea kushikilia sehemu kubwa ya deni la ndani la Serikali, huku benki za biashara na mifuko ya hifadhi za jamii zikiendelea kuwa wakopeshaji (wadai) wakuu (Jedwali 2.6.5 na 2.6.6).

**Kielelezo 2.6.1: Deni la Ndani la Serikali Kuu**

Shilingi Bilioni




Chanzo: Wizara ya Fedha

**Jedwali 2.6.5: Deni la Ndani la Serikali Kuu kwa Vyanzo vya Mkopo**

Shilingi Bilioni

| | Jul-24 | | Jun-25 | | Jul-25ᴾ | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) |
| Dhamana za serikali | 27,594.5 | 84.0 | 30,170.4 | 85.0 | 30,342.5 | 85.8 |
| Dhamana za serikali za muda mfupi | 2,128.9 | 6.5 | 2,001.3 | 5.6 | 2,016.9 | 5.7 |
| Hisa za serikali | 187.1 | 0.6 | 187.1 | 0.5 | 135.7 | 0.4 |
| Dhamana za serikali za muda mrefu | 25,278.5 | 77.0 | 27,982.0 | 78.8 | 28,189.8 | 79.7 |
| Vyeti vya ushuru | 0.1 | 0.0 | 0.1 | 0.0 | 0.1 | 0.0 |
| Deni lisilo na dhamana | 5,244.6 | 16.0 | 5,332.4 | 15.0 | 5,008.9 | 14.2 |
| Madeni mengine* | 18.4 | 0.1 | 18.4 | 0.1 | 18.4 | 0.1 |
| Bakaa hasi | 5,226.2 | 15.9 | 5,314.0 | 15.0 | 4,990.5 | 14.1 |
| Deni la ndani (ukiondoa karatasi za ukwasi) | 32,839.1 | 100.0 | 35,502.8 | 100.0 | 35,351.4 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha, na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: p inamaanisha takwimu za awali; na madeni mengine yanajumuisha mkopo wa kawaida wa NMB na marejesho ya kodi ya ushuru

**Jedwali 2.6.6: Deni la Ndani la Serikali Kuu Kwa Kundi la Wakopeshaji**

Shilingi Bilioni

| | Jul-24 | | Jun-25 | | Jul-25ᴾ | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mkopeshaji | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) |
| Benki za biashara | 9,796.5 | 30.2 | 10,161.5 | 28.6 | 10,176.3 | 28.8 |
| Benki Kuu ya Tanzania | 7,186.3 | 22.1 | 7,174.1 | 20.2 | 6,799.3 | 19.2 |
| Mifuko ya hifadhi ya jamii | 8,780.4 | 27.0 | 9,265.7 | 26.1 | 9,328.8 | 26.4 |
| Kampuni za Bima | 1,853.2 | 5.7 | 1,843.0 | 5.2 | 1,808.4 | 5.1 |
| Mifuko maalumu ya BoT | 321.2 | 1.0 | 638.1 | 1.8 | 777.3 | 2.2 |
| Wengine | 4,540.6 | 14.0 | 6,420.4 | 18.1 | 6,461.3 | 18.3 |
| Deni la ndani (ukiondoa karatasi za ukwasi) | 32,478.1 | 100.0 | 35,502.8 | 100.0 | 35,351.4 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha, na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: BOT inamaanisha Benki Kuu ya Tanzania; p, takwimu za awali; na "wengine" inajumuisha taasisi za umma, kampuni na watu binafsi

Mwezi Julai 2025, Serikali ilikopa jumla ya shilingi bilioni 514.5 kutoka soko la ndani kupitia utoaji wa

dhamana za Serikali, kwa lengo la kufadhili nakisi ya bajeti (Kielelezo 2.6.2). Wakati huo huo, Serikali ilitumia jumla ya shilingi bilioni 670.8 kulipia deni la ndani, ambapo shilingi bilioni 342.3 zilitumika kwa malipo ya mkopo mkuu na shilingi bilioni 328.5 kwa malipo ya riba.

**Kielelezo 2.6.2: Dhamana za Serikali Zilizotolewa kwa Madhumuni ya Ufadhili wa Bajeti**

Shilingi Bilioni




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Deni la ndani la baadhi ya mashirika ya umma (SOEs) ni shilingi bilioni 83.9 ambapo hakukuwa na mabadiliko yoyote kutoka kiasi kilichorekodiwa mwezi uliopita (Jedwali 2.6.7).

**Jedwali 2.6.7: Deni la Ndani la Baadhi ya Mashirika ya Umma**

Shilingi Bilioni

| | Jul-24 | | Jun-25 | | Jul-25 | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) |
| Shirika la Umeme Tanzania | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Shirika la Ndege Tanzania | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Kampuni ya Mbolea Tanzania | 20.4 | 26.9 | 20.4 | 24.3 | 20.4 | 24.3 |
| Mamlaka ya Bandari | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| DAWASA | 50.7 | 66.8 | 57.8 | 69.0 | 57.7 | 68.9 |
| Shirika la Reli Tanzania | 4.8 | 6.3 | 5.6 | 6.7 | 5.7 | 6.8 |
| Total | 76.0 | 100.0 | 83.9 | 100.0 | 83.9 | 100.0 |

Chanzo: Ofisi ya Msajili wa Hazina
Tanbihi: DAWASA inamaanisha Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam

## 2.7 Mwenendo wa Sekta ya Nje

Sekta ya nje iliendelea kuimarika katika mwaka ulioishia Julai 2025, ambapo nakisi ya urari wa malipo ya kawaida ilipungua hadi kufikia dola za Marekani milioni 2,079.2 kutoka dola za Marekani milioni 2,713.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2024 (Jedwali 2.7.1). Mwenendo huu ulichangiwa na kuongezeka kwa ziada ya biashara iliyotokana na ukuaji wa mauzo ya nje ya bidhaa na huduma ikilinganishwa na uagizaji. Hali hii inaashiria kuimarika kwa ushindani wa sekta ya nje na kuongekezeka kwa mahitaji ya bidhaa za ndani katika masoko ya kimataifa.

Akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani milioni 6,194.4 mwishoni mwa mwezi Julai 2025, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 5,292.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Kiwango hiki kinatosha kugharamia uagizaji wa bidhaa na huduma kwa miezi mitano, juu ya lengo la kitaifa la miezi minne na la Jumuiya ya Afrika Mashariki (Kielelezo 2.7.1).

**Jedwali 2.7.1 Urari wa Malipo ya Kawaida**

Dola za Marekani Milioni

| | Jul-24 | Jun-25 | Jul-25 | Mwaka ulioishia Julai 2023 | 2024 | 2025 | Mabadiliko ya asilimia |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Urari wa bidhaa | -238.5 | -395.8 | -548.3 | -6,715.0 | -5,927.4 | -5,240.9 | -11.6 |
| Zilozouzwa nje* | 847.1 | 881.8 | 551.3 | 7,495.8 | 7,918.2 | 9,479.4 | 19.7 |
| Zilizonunuliwa nje | 1,085.6 | 1,277.6 | 1,099.6 | 14,210.8 | 13,845.6 | 14,720.3 | 6.3 |
| Urari wa huduma | 425.78 | 430.1 | 354.5 | 2,961.5 | 4,229.4 | 4,250.5 | 0.5 |
| Mapato | 656.4 | 695.2 | 595.6 | 5,510.1 | 6,643.8 | 7,175.6 | 8.0 |
| Malipo | 230.6 | 265.1 | 241.2 | 2,548.6 | 2,414.5 | 2,925.1 | 21.2 |
| Urari wa bidhaa na huduma | 187.3 | 34.3 | -193.8 | -3,753.5 | -1,698.0 | -990.4 | -41.7 |
| Bidhaa na huduma zilizouzwa nje | 1,503.4 | 1,577.0 | 1,147.0 | 13,005.9 | 14,562.0 | 16,655.0 | 14.4 |
| Bidhaa na huduma zilizonunuliwa kutoka nje | 1,316.2 | 1,542.7 | 1,340.8 | 16,759.4 | 16,260.0 | 17,645.4 | 8.5 |
| Urari wa malipo wa vitega uchumi | -116.1 | -153.6 | -197.8 | -1,446.0 | -1,638.7 | -1,818.8 | 11.0 |
| Yaliyoingia | 29.0 | 29.5 | 46.2 | 219.6 | 336.7 | 411.2 | 22.1 |
| Yaliyotoka | 145.1 | 183.0 | 244.0 | 1,665.6 | 1,975.4 | 2,230.0 | 12.9 |
| Urari wa uhamisho mali ya kawaida | 50.0 | 47.0 | 110.6 | 638.6 | 623.2 | 730.0 | 17.1 |
| Iliyoingia | 95.5 | 71.3 | 157.1 | 973.3 | 1,290.7 | 1,158.9 | -10.2 |
| ambapo Serikali | 6.3 | 0.0 | 80.9 | 85.9 | 129.0 | 171.2 | 32.7 |
| Iliyotoka | 45.4 | 24.2 | 46.5 | 334.7 | 667.5 | 428.9 | -35.7 |
| Urari wa Bidhaa, Huduma na Uhamisho Mali | 121.2 | -72.2 | -281.0 | -4,560.9 | -2,713.5 | -2,079.2 | -23.4 |

Chanzo*:* Mamlaka ya Mapato Tanzania, Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi*:* a- inamaanisha takwimu za awali *Zinajumuisha marekebisho kwa ajili ya mauzo nje ya nchi yasiyorekodiwa

**Kielelezo 2.7.1 Akiba ya Fedha za Kigeni**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: LHS Inaashiria skeli ya mhimili wa Kushoto; RHS, Inaashiria skeli ya mhimili wa Kulia.

## Mauzo ya Nje

Katika mwaka ulioishia Julai 2025, mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yaliongezeka kwa asilimia 14 na kufikia dola za Marekani milioni 16,655. Ongezeko hili lilichangiwa na mapato ya utalii, mauzo ya dhahabu na bidhaa asilia.

Mauzo ya bidhaa yaliongezeka kwa asilimia 19.7 na kufikia dola za Marekani milioni 9,479.4 katika mwaka ulioishia Julai 2025 (Kielelezo 2.7.2). Vichocheo vikuu vya ongezeko hilo vilikuwa dhahabu, korosho, mazao ya mbogamboga, kahawa na nafaka, hususan mahindi na mchele yaliyouzwa nchi jirani. Thamani ya mauzo ya dhahabu iliongezeka hadi kufikia dola za Marekani milioni 3,977.6 kutoka dola za Marekani milioni 3,148, ongezeko lilitokana na bei nzuri katika masoko ya kimataifa na kuongezeka kwa uzalishaji. Mauzo ya bidhaa za asilia yalifikia dola za Marekani milioni 1,388 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,074.4, ambapo korosho na kahawa zilichangia zaidi kutokana na kuongezeka kwa bei na kiasi kilichouzwa. Mauzo ya nafaka yaliongezeka zaidi ya mara mbili na kufikia dola za Marekani milioni 382.3, yakichangiwa zaidi na mauzo ya mahindi na mchele kutokana na kuongezeka kwa mahitaji nchi jirani. Kwa ulinganifu wa mwezi, mauzo ya bidhaa nje ya nchi kwa mwezi Julai 2025 yalifikia dola milioni 551.3, ikilinganishwa na dola milioni 847.1 mwezi Julai 2024.

**Kielelezo 2.7.2: Mauzo ya Nje ya Bidhaa na Huduma**
Dola za Marekani Milioni




Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: p- inamaanisha takwimu za awali

Mapato ya huduma yaliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 7,175.6 katika mwaka ulioishia Julai 2025, kutoka dola za Marekani milioni 6,643.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Ukuaji huu ulichangiwa zaidi na ongezeko la mapato ya utalii na usafirishaji. Mapato ya utalii yaliongezeka kwa asilimia 3.8 na kufikia dola za Marekani milioni 3,871.9, sambamba na kuongezeka kwa idadi ya watalii hadi 2,249,387 kutoka 2,026,378 katika kipindi kama hicho mwaka uliopita (Kielelezo 2.7.3).

**Kielelezo 2.7.3: Mapato ya Huduma kwa Sekta**
Dola za Marekani Milioni




Chanzo*:* Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: p inamaanisha takwimu za awali.Huduma zingine huusisha ujenzi, bima na fedha, mawasiliano, Habari na tekinolojia, mrabaha wa matumizi ya hati miliki, huduma za kiserikali, huduma binafsi na za kibiashara.

## Uagizaji wa Bidhaa

Uagizaji wa bidhaa na huduma ulifikia dola za Marekani milioni 17,645.4 katika mwaka ulioishia Julai 2025, kutoka dola za Marekani milioni 16,260 katika kipindi kama hicho mwaka 2024 (Jedwali 2.7.2). Ongezeko hili lilitokana hasa na ongezeko la uagizaji wa vifaa vya usafirishaji, malighafi za viwandani, bidhaa za chuma, pamoja na vifaa. Katika kipindi husika, uagizaji wa mafuta (hususan bidhaa za petroli zilizochujwa) ulipungua hadi dola za Marekani milioni 2,689.1 kutoka dola za Marekani milioni 2,846.1. Hii ilitokana na kushuka kwa bei ya bidhaa hiyo katika soko la dunia, ambayo ilipungua kwa asilimia 14.2 na kufikia wastani wa dola za Marekani 71.6 kwa pipa. Kwa mwezi wa Julai 2025, uagizaji wa bidhaa ulifikia dola za Marekani milioni 1,099.6 ikilinganishwa na dola milioni 1,085.6 mwezi Julai 2024.

**Kielelezo 2.7.4: Uagizaji wa Bidhaa na Huduma**

Dola za Marekani Milioni




Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

Tanbihi: p inamaanisha takwimu za awali.

Malipo ya huduma yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 2,925.1 katika mwaka ulioishia Julai 2025, kutoka dola milioni 2,414.5 mwaka 2024, kutokana na kuongezeka kwa gharama za usafirishaji wa mizigo na ongezeko la uagizaji wa bidhaa (Kielelezo 2.7.5). Kwa mwezi wa Julai 2025, malipo ya huduma yalifikia dola za Marekani milioni 241.2, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 230.6 kwa mwezi Julai 2024.

**Kielelezo 2.7.5: Malipo ya Huduma**

Dola za Marekani Milioni




Chanzo: Benki na Benki Kuu ya Tanzania

Tanbihi: p inamaanisha takwimu za awali. Huduma nyingine zinajumuisha ujenzi, bima, huduma za kifedha, mawasiliano, kompyuta na taarifa, ada za matumizi ya haki miliki, huduma za serikali, binafsi na huduma nyingine za kibiashara

Nakisi ya urari wa mapato ya vitega uchumi iliongezeka hadi dola za Marekani milioni 1,818.8 katika mwaka ulioishia Julai 2025, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,638.7 katika kipindi kama hicho mwaka uliopita. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa malipo ya gawio na riba. Kwa mwezi wa Julai 2025, nakisi ya urari wa vitega uchumi ilikuwa dola za Marekani milioni 197.8, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 116.1 mwezi Julai 2024.

Urari wa uhamisho wa mali za kawaida ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 730, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 623.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2024, kutokana na kuongezeka kwa uhamisho wa fedha binafsi. Kadhalika, mwezi Julai 2025 ulirekodi ziada ya dola za Marekani milioni 110.6 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 50 mwezi Julai 2024.

# 3.0 Mwenendo wa Uchumi wa Zanzibar

## 3.1 Mfumuko wa Bei

Mfumuko wa bei wa jumla kwa mwaka ulipungua hadi asilimia 4.1 mwezi Julai 2025, kutoka asilimia 5.3 mwezi uliopita, na asilimia 5.3 katika mwezi kama huo mwaka 2024 (Jedwali 3.1.1). Kupungua huko kulichangiwa zaidi na kushuka kwa mfumuko wa bei ya chakula kufuatia kupungua kwa bei za mchele, sukari, unga na ndizi, ikiashiria upatikanaji wa kutosha wa bidhaa hizi sokoni. Kwa kipimo cha mwezi hadi mwezi, mfumuko wa bei wa jumla ulikuwa asilimia 0.2 mwezi Julai 2025, kutoka asilimia 0.5 mwezi Juni 2025. Mfumuko wa bei mwezi Julai 2025 ulikuwa sawa na wa mwezi Julai 2024.

### Jedwali 3.1.1: Mwenendo wa mfumuko wa bei

Kizio: Julai 2022 =100

| Kundi | Uzito | Mabadiliko kila Mwezi Jul-24 | Jun-25 | Jul-25 | Mabadiliko kwa mwaka unaoishia Jun-25 | Jul-25 | Jul-25 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Vyakula na Vinywaji Visivyo na Kileo | 41.9 | 0.2 | 1.1 | 0.1 | 9.0 | 5.0 | 4.9 |
| Vinywaji vyenye Vileo, Tumbaku na Madawa ya binadamu | 0.2 | 0.7 | 0.0 | 4.9 | 24.6 | -2.2 | 3.4 |
| Mavazi na Viatu | 6.3 | 0.1 | 0.2 | 0.1 | 0.7 | 5.0 | 5.1 |
| Makazi, Maji, Umeme, Gesi na Nishati Nyingine | 25.8 | 0.6 | -0.1 | 0.4 | 3.2 | 3.6 | 3.4 |
| Matengenezo ya Kawaida ya Nyumba | 4.8 | 0.0 | 0.0 | 0.5 | 1.5 | 3.8 | 4.3 |
| Afya | 1.3 | 0.0 | 0.0 | 0.1 | -3.1 | 1.5 | 1.6 |
| Uchukuzi | 9.1 | -0.1 | 0.0 | -0.1 | 3.1 | 2.4 | 2.3 |
| Taarifa na mawasiliano | 4.2 | 0.1 | 0.7 | 0.0 | 1.6 | 2.8 | 2.7 |
| Burudani, Michezo na Utamaduni | 1.1 | 0.0 | 0.6 | -0.8 | 4.0 | 5.1 | 4.3 |
| Elimu | 1.6 | 0.0 | -1.6 | 1.7 | -7.7 | 2.1 | 3.8 |
| Huduma za Migahawa na Malazi | 1.4 | 0.0 | 0.0 | 1.0 | 11.7 | 0.6 | 1.6 |
| Bima na Huduma za Fedha | 0.5 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Huduma binafsi, Ulinzi wa Kijamii na Bidhaa na Huduma Mbalimbali | 1.7 | 0.0 | 0.0 | 0.1 | 1.6 | 4.8 | 5.0 |
| Mfumuko wa bei wa jumla | 100.0 | 0.2 | 0.5 | 0.2 | 5.3 | 4.1 | 4.1 |
| Mfumuko wa bei wa bidhaa za chakula | 40.5 | 0.2 | 1.2 | 0.1 | 9.2 | 4.4 | 4.3 |
| Mfumuko wa bei wa bidhaa zisizo za chakula | 59.5 | 0.3 | 0.0 | 0.3 | 2.4 | 3.9 | 3.9 |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

### Kielelezo 3.1.1: Mabadiliko ya mfumuko wa bei katika asilimia

Asilimia




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

## 3.2 Shughuli za Bajeti ya Serikali

Mwezi Julai 2025, mapato ya ndani ya Serikali pamoja na misaada yalifikia shilingi bilioni 176.2, kiwango kilichozidi lengo kwa asilimia 20.3. Katika kiasi hiki, Shilingi bilioni 150.1 yalikuwa mapato ya ndani na kiasi kilichobaki kilikuwa misaada. Mapato ya kodi yalifikia shilingi bilioni 133.3, zaidi ya lengo kwa asilimia 5.2, ambapo makundi yote ya kodi yalivuka matarajio. Mapato yasiyotokana na kodi yalikuwa shilingi bilioni 16.8, sawa na asilimia 85.0 ya lengo (Kielelezo 3.2.1).

### Kielelezo 3.2.1: Mapato ya Serikali

Shilingi Bilioni




Chanzo: Ofisi ya Raisi, Mipango na Fedha, Zanzibar
Tanbihi: Kodi nyingine zinahusisha tozo za hoteli, tozo za wasindikiza wageni, stampu za tozo, tozo za huduma za viwanja vya ndege na bandari, tozo za maendeleo ya barabara na petroli

Matumizi ya Serikali yalifikia shilingi bilioni 200.7 mwezi Julai 2025. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 160.4 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na shilingi bilioni 40.3 zikielekezwa kwenye matumizi ya miradi ya maendeleo (Kielelezo 3.2.2). Mikopo ya ndani ilitumika kujaza upungufu wa shilingi bilioni 24.5 wa bajeti.

### Kielelezo 3.2.2: Matumizi ya Serikali

Shilingi Bilioni




Chanzo: Ofisi ya Raisi, Mipango na Fedha, Zanzibar
Tanbihi: Matumizi mengine yanahusisha uhamisho wa fedha, malipo ya riba ya deni la ndani, huduma za mfuko mkuu wa serikali na tozo zingine.

## 3.3 Mwenendo wa Sekta ya Nje

### Urari wa Malipo ya Kawaida

Urari wa Malipo ya kawaida uliongezeka kwa asilimia 34.7 hadi kufikia dola za Marekani milioni 558.5 mwaka ulioishia Julai 2025, kutoka ziada ya dola milioni 414.8 iliyorekodiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Ongezeko la urari huu limechangiwa

na mapato ya huduma zinazohusiana na shughuli za kitalii (Jedwali 3.3.1).

### Jedwali 3.3.1: Urari wa malipo

Dola za Marekani Milioni

| Maelezo | Jul-24 | Jun-25 | Jul-25$^P$ | Mwaka unaoishia Julai 2024 | Mwaka unaoishia Julai 2025$^p$ | Ongezeko/ Upungufu (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Urari wa bidhaa (Halisi) | -35.6 | -42.4 | -43.2 | -408.6 | -450.6 | 10.3 |
| Zilizouzwa nje | 2.9 | 1.6 | 1.7 | 64.3 | 32.1 | -50.1 |
| zilizonunuliwa kutoka nje | 38.5 | 44.0 | 44.9 | 473.0 | 482.7 | 2.1 |
| Urari wa huduma (halisi) | 89.3 | 84.0 | 131.9 | 773.5 | 1,076.1 | 39.1 |
| Mapato | 96.9 | 87.5 | 139.9 | 858.6 | 1,177.4 | 37.1 |
| Malipo | 7.5 | 3.5 | 7.9 | 85.1 | 101.3 | 19.0 |
| Urari wa bidhaa na huduma (halisi) | 53.7 | 41.6 | 28.8 | 400.5 | 537.5 | 34.2 |
| Bidhaa na huduma zilizouzwa nje | 99.7 | 89.1 | 141.6 | 923.0 | 1,209.5 | 31.0 |
| Bidhaa na huduma zilizonunuliwa kutoka nje | 46.0 | 47.5 | 52.8 | 558.0 | 584.0 | 4.7 |
| Urari wa mapato ya msingi (halisi) | 1.5 | 2.2 | 2.2 | 12.6 | 18.5 | 47.2 |
| Yaliyoingia | 2.2 | 3.2 | 3.2 | 18.3 | 26.9 | 47.1 |
| Yaliyotoka | 0.7 | 1.0 | 1.0 | 5.8 | 8.5 | 47.0 |
| Urari wa uhamishaji Mali (halisi) | 0.2 | 0.3 | 0.3 | 1.8 | 2.6 | 46.3 |
| Iliyoingia | 0.4 | 0.5 | 0.5 | 3.0 | 4.5 | 46.3 |
| Iliyotoka | 0.2 | 0.2 | 0.2 | 1.3 | 1.9 | 46.3 |
| Urari wa Bidhaa,huduma na uhamishaji mali | 55.5 | 44.1 | 31.4 | 414.8 | 558.5 | 34.7 |

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania, benki na uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania.
Tanbihi: p inaashiria Takwimu za awali; fob, 'freight on board'.

## Uuzaji wa Bidhaa Nje

Mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yaliongezeka kwa asilimia 31.0 hadi kufikia dola za Marekani milioni 923.0 mwaka ulioishia Julai 2024. Mafanikio haya yalichangiwa kwa kiasi kikubwa na mapato ya huduma, hususan kutoka sekta ya utalii, ambayo yalipanda kutoka asilimia 37.1 hadi dola milioni 1,177.4 kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watalii. Idadi ya watalii walioingia nchini iliongezeka hadi 828,752 kutoka 672,956 waliorekodiwa mwaka ulioishia Julai 2024 (Jedwali 3.3.2). Kwa upande mwingine, thamani ya mauzo ya karafuu nje ya nchi ilipungua kwa asilimia 87.6, hadi dola za Marekani milioni 3.6 kutoka dola za Marekani milioni 28.8, kutokana uzalishaji mdogo unaosababishwa na tabia ya mzunguko wa mavuno wa zao hilo (*cyclical nature*). Hata hivyo, kwa ulinganifu wa kila mwezi, mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yalipungua hadi dola za Marekani milioni 81.7 kutoka dola za Marekani milioni 99.7 zilizorekodiwa mwezi Julai 2024.

### Jedwali 3.3.2: Uuzaji wa Bidhaa

Dola za Marekani Milioni

| Maelezo | Uniti | Jul-24 | Jun-25 | Jul-25$^P$ | Mwaka unaoishia Julai 2024 | Mwaka unaoishia Julai 2025$^p$ | Ongezeko/Upungufu (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mauzo ya nje ya bidhaa za asili | | | | | | | |
| Karafuu | | | | | | | |
| Thamani | 000' | 0.3 | 136.1 | 123.8 | 28,750.6 | 3,574.0 | -87.6 |
| Kiasi | 000' kwa Tani | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 4.3 | 0.8 | -82.1 |
| Bei kwa Unit | USD/Tani | 6,500.0 | 4,372.5 | 4,001.1 | 4,129.8 | 4,144.1 | 0.3 |
| Mauzo ya nje ya bidhaa zisizo za asili | | | | | - | 0.0 | |
| Mwani | | | | | - | 0.0 | |
| Thamani | 000' | 136.6 | 302.2 | 277.9 | 5,924.5 | 3,363.2 | -43.2 |
| Kiasi | 000' kwa Tani | 0.3 | 0.5 | 0.5 | 9.0 | 6.0 | -32.5 |
| Bei kwa Unit | USD/Tani | 517.2 | 567.7 | 548.8 | 7,739.6 | 6,472.7 | -16.4 |
| Bidhaa za Viwandani | 000' | 291.6 | 816.5 | 892.8 | 18,424.5 | 15,991.3 | -13.2 |
| Bidhaa za samaki | 000' | 200.1 | 38.8 | 47.2 | 2,130.3 | 1,023.4 | -52.0 |
| Mauzo ya nje ya nchini kwa bidhaa nyingine | 000' | 2,250.8 | 319.4 | 348.4 | 9,116.1 | 8,152.1 | -10.6 |
| Jumla Ndogo | 000' | 2,879.1 | 1,476.9 | 1,566.3 | 35,595.4 | 28,530.0 | -19.8 |
| Jumla Kuu | 000' | 2,879.4 | 1,613.0 | 1,690.1 | 64,346.0 | 32,104.0 | -50.1 |

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania.

## Uagizaji wa Bidhaa

Uagizaji wa bidhaa na huduma katika mwaka ulioishia Julai 2025 uliongezeka kwa asilimia 4.7 hadi kufikia Dola za Marekani milioni 584.0. Kiasi hiki ni ongezeko la dola za Marekani milioni 558.0 zilizorekodiwa katika kipindi kama hicho cha mwaka uliopita (Jedwali 3.3.1). Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa za matumizi na za mitaji.

Uagizaji wa bidhaa za matumizi uliongezeka kwa asilimia 2.5 hadi kufikia Dola za Marekani milioni 50.3, kutoka Dola za Marekani milioni 49.1, hali iliyochangiwa zaidi na kuongezeka kwa uagizaji wa vifaa vya viwandani zinazotumia umeme na bidhaa zingine. Vivyo hivyo, uagizaji wa bidhaa za mitaji uliongezeka kwa asilimia 2.4 hadi kufikia Dola za Marekani milioni 59.1 kutokana na kuongezeka kwa uagizaji wa vifaa tiba na bidhaa nyingine (Jedwali 3.3.3). Kwa kila mwezi, uagizaji wa bidhaa na huduma uliongezeka kufikia Dola za Marekani milioni 52.8 kutoka Dola milioni 46.0 zilizorekodiwa mwezi July 2024.

## Jedwali 3.3.3: Uagizaji wa Bidhaa

Dola za Marekani Milioni

| Maelezo | Jul-24 | Jun-25 | Jul-25P | Mwaka unaoishia Julai 2024 | Mwaka unaoishia Julai 2025p | Ongezeko/ Upungufu (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Bidhaa za Mtaji | 6.5 | 4.4 | 4.8 | 49.1 | 50.3 | 2.5 |
| Mitambo na vifaa vya kimitambo | 2.0 | 1.6 | 1.9 | 14.1 | 14.5 | 3.3 |
| Vifaa vya usafirishaji Kiwandani | 1.6 | 1.2 | 1.3 | 18.0 | 17.7 | -1.8 |
| Mashine na Vifaa vya Umeme | 1.6 | 0.9 | 1.0 | 9.1 | 10.5 | 14.7 |
| Bidhaa nyingine za mtaji | 1.3 | 0.6 | 0.6 | 7.8 | 7.6 | -3.5 |
| Bidhaa za uzalishaji wa kati | 26.6 | 34.2 | 34.6 | 366.2 | 373.4 | 2.0 |
| Vifaa vya viwandani | 9.8 | 10.3 | 11.2 | 99.2 | 98.8 | -0.4 |
| Ambazo ni chuma na bidhaa zinazotokana navyo | 1.5 | 1.8 | 2.0 | 22.8 | 24.0 | 5.1 |
| Plastiki na bidhaa zake | 0.5 | 0.6 | 0.6 | 5.9 | 5.7 | -3.4 |
| Mbolea | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.1 | 0.1 | 0.0 |
| Nishati na mafuta | 11.4 | 14.0 | 13.3 | 182.1 | 185.0 | 1.6 |
| ambazo ni bidhaa safi za mafuta | 11.0 | 14.0 | 13.3 | 180.9 | 183.4 | 1.4 |
| Vifaa | 1.8 | 1.1 | 1.2 | 14.7 | 14.0 | -4.6 |
| Chakula na Vinywaji kwa Matumizi ya Viwandani | 1.5 | 7.4 | 7.3 | 55.5 | 60.8 | 9.5 |
| ambazo ni nafaka ya ngano | 0.0 | 2.2 | 2.0 | 16.5 | 20.5 | 24.1 |
| Mafuta ya kula | 1.4 | 3.6 | 3.5 | 21.4 | 23.5 | 10.2 |
| Sukari kwa Matumizi ya Viwandani | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | -0.7 |
| Magari ya matumizi ya nyumbani | 2.1 | 1.4 | 1.6 | 14.7 | 14.8 | 0.8 |
| Bidhaa za Matumizi ya Mwisho | 5.4 | 5.4 | 5.5 | 57.7 | 59.1 | 2.4 |
| Chakula na vinywaji vinavyotumika hasa kwa matumizi ya n | 1.3 | 1.3 | 1.3 | 13.6 | 13.9 | 2.1 |
| Vifaa vya Usafirishaji Visivyo vya Viwandani | 0.2 | 0.2 | 0.2 | 1.7 | 1.7 | -3.1 |
| ambazo ni pikipiki na baiskeli zilizowekwa na mota ndogo y | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.7 | 0.7 | 2.3 |
| Bidhaa nyingine za matumizi ya mwisho | 3.9 | 3.9 | 0.2 | 42.3 | 43.5 | 2.7 |
| ambazo ni bidhaa za dawa | 0.0 | 0.4 | 0.4 | 1.4 | 1.6 | 9.3 |
| Dawa za kuua wadudu na bidhaa zinazofanana | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.5 | 0.4 | -4.1 |
| Sabuni na dawa za kusafisha | 0.5 | 0.3 | 182.1 | 3.2 | 3.3 | 3.2 |
| Vitambaa na Mavazi | 0.5 | 0.4 | 0.4 | 5.3 | 5.4 | 3.0 |
| Viatu na bidhaa nyingine | 0.2 | 0.2 | 0.2 | 2.0 | 2.0 | -1.7 |
| Karatasi na bidhaa zake | 0.1 | 0.2 | 0.2 | 2.1 | 2.2 | 5.0 |
| Jumla (f.o.b) | 38.5 | 44.0 | 44.9 | 473.0 | 482.7 | 2.1 |

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania.

Tanbihi: p inaashiria takwimu za awali; “---“, badiliko linalozidi asilimia 100; f.o.b Mzigo ndani ya chombo

# Viambatisho

## Jedwali A1: Viashiria vya Kiuchumi

| | | 2020 | 2021 | 2022 | 2023[r] | 2024[p] |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Ukuaji wa Pato la Taifa na Mfumuko wa bei | | | | | | |
| 1.1 Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Bei za Miaka Husika | Asilimia | 8.1 | 7.4 | 9.4 | 10.5 | 9.6 |
| 1.2 Ukuaji halisi wa Pato la Taifa | Asilimia | 4.5 | 4.8 | 4.7 | 5.1 | 5.5 |
| 1.3 Wastani Pato kwa Kila Mtu kwa bei za miaka inayohusika | '000' Sh. | 2,597.7 | 2,705.4 | 2,854.1 | 3,058.8 | na |
| 1.4 Wastani Pato kwa Kila Mtu kwa bei za miaka inayohusika | Dola ya Marekani | 1,132.3 | 1,177.4 | 1,239.3 | 1,284.1 | na |
| 1.5 Kasi ya Upandaji Bei | Asilimia | 3.3 | 3.7 | 4.3 | 3.8 | 3.1 |
| 1.6 Uwiano wa Akiba kwa Pato halisi la Taifa (net national disposable income) | Asilimia | 16.5 | 17.3 | 19.7 | 21.9 | na |
| Takwimu za Kifedha na Riba | | | | | | |
| 2.1 Ukuaji wa Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) | Asilimia | 5.7 | 15.5 | 11.6 | 14.1 | 11.1 |
| 2.2 Ukuaji wa Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) | Asilimia | 8.2 | 17.6 | 12.1 | 11.9 | 9.2 |
| 2.3 Ukuaji wa Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1) | Asilimia | 7.5 | 23.1 | 7.5 | 8.7 | 11.2 |
| 2.4 Ukuaji Fedha ya msingi (M0) | Asilimia | -4.0 | 17.3 | 15.8 | 3.7 | 19.1 |
| 2.5 Ukuaji wa Mikopo kwa Sekta Binafsi | Asilimia | 3.1 | 10.0 | 22.5 | 17.3 | 12.4 |
| 2.6 Uwiano wa Mikopo kwa Sekta Binafsi kwa pato la taifa[1] | Asilimia | 14.0 | 14.3 | 16.0 | 17.0 | 17.4 |
| 2.7 Uwiano wa Mikopo kwa sekta binafsi kwa mikopo yote | Asilimia | 77.7 | 74.4 | 72.9 | 73.9 | 75.9 |
| 2.8 Riba za Amana za miezi 12 | Asilimia | 8.3 | 8.3 | 8.5 | 8.7 | 9.2 |
| 2.9 Riba za dhamana za serikali kwa ujumla | Asilimia | 4.4 | 4.8 | 4.7 | 7.3 | 10.7 |
| 2.10 Riba ya mikopo ya muda mrefu hadi miaka mitano (3-5 years) | Asilimia | 16.2 | 16.0 | 15.7 | 15.6 | 15.3 |
| Mizania ya Malipo na Nchi za Nje | | | | | | |
| 3.1 Bidhaa Zilizouzwa Nje | Dola Millioni | 6,371.7 | 6,756.2 | 7,223.8 | 7,696.6 | 9,121.6 |
| 3.2 Bidhaa Zilizoagizwa kutoka Nje ya Nchi | Dola Millioni | -7,831.7 | -10,003.4 | -14,208.7 | -13,728.9 | -14,278.9 |
| 3.3 Urari wa Biashara | Dola Millioni | -1,460.0 | -3,247.1 | -6,984.9 | -6,032.3 | -5,157.2 |
| 3.4 Urari wa Malipo ya Kawaida | Dola Millioni | -1,458.5 | -2,374.3 | -5,482.2 | -2,960.6 | -2,032.0 |
| 3.5 Urari wa malipo yote | Dola Millioni | -764.9 | 1,852.1 | -988.4 | 52.3 | 80.5 |
| 3.6 Akiba ya Fedha za Kigeni | Dola Millioni | 4,767.7 | 6,386.0 | 5,177.2 | 5,450.1 | 5,546.9 |
| 3.7 Akiba ya fedha za kigeni (miezi) | Miezi | 5.6 | 6.6 | 4.7 | 4.5 | 4.5 |
| 3.8 Kiwango cha kubadili fedha: | | | | | | |
| Wastani wa mwaka | Thamani ya Tshs/Dola | 2,294.1 | 2,297.8 | 2,303.1 | 2,382.1 | 2,597.3 |
| Mwisho wa kipindi | Thamani ya Tshs/Dola | 2,298.5 | 2,297.6 | 2,308.9 | 2,501.4 | 2,374.7 |
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 |
| Mwenendo wa Mapato na Matumizi | | | | | | |
| 4.1 Uwiano wa mapato ya ndani kwa Pato la Taifa[1] | Asilimia | 15.0 | 13.7 | 14.9 | 15.0 | 15.0 |
| 4.2 Uwiano wa misaada kwa Pato la Taifa[1] | Asilimia | 0.7 | 0.5 | 0.4 | 0.3 | 0.3 |
| 4.3 Uwiano wa Matumizi ya kawaida kwa Pato la Taifa[1] | Asilimia | 10.1 | 9.9 | 9.8 | 11.0 | 11.0 |
| 4.4 Uwiano wa matumizi ya maendeleo kwa Pato la Taifa[1] | Asilimia | 7.1 | 7.8 | 9.2 | 7.4 | 7.4 |
| 4.5 Uwiano wa nakisi isiyojumuisha misaada kwa Pato la Taifa[1] | Asilimia | -2.2 | -4.0 | -4.1 | -3.4 | -3.4 |
| 4.6 Uwiano wa nakisi ya Jumla kwa Pato la Taifa[1,2] | Asilimia | -1.9 | -4.0 | -3.6 | -3.1 | -3.1 |
| Deni la nje | Dola Millioni | 22,952.7 | 25,519.3 | 27,832.5 | 30,252.7 | 31,950.9 |
| 5.1 Mikopo iliyopokelewa | Dola Millioni | 20,958.4 | 23,250.9 | 25,392.8 | 27,889.3 | 30,416.1 |
| 5.2 Riba ambayo haijalipwa | Dola Millioni | 1,994.3 | 2,268.4 | 2,439.7 | 2,363.4 | 1,534.8 |

Chanzo: Wizara ya Fedha; Benki kuu ya Tanzania; na Mamlaka ya mapato Tanzania

Tanbihi: [1] Imekokotolewa kwa kuzingatia Pato la Taifa kwa bei za miaka husika; [2] inajumuisha misaada, matumizi yaliyochelewa (expenditure float)

n.a - haipatikani, p - ni takwimu za muda

**Jedwali A2: Mwenendo wa Mapato na Matumizi ya Serikali – Tanzania Bara**

Shilingi Milioni

| | Bajeti ya | Julai 2024 - Juni 2025 | | Juni-25 | |
|---|---|---|---|---|---|
| | 2024/25 | Makadirio | Halisi | Makadirio | Halisi |
| Mapato ya ndani (yakijumuisha Mamlaka za Serikali za Mitaa) | 34,610,646.4 | 34,491,408.1 | 34,847,444.7 | 3,571,808.0 | 3,753,392.8 |
| Mapato ya Serikali Kuu | 33,254,305.8 | 33,135,067.5 | 33,408,589.5 | 3,444,267.1 | 3,579,197.2 |
| Mapato yatokanayo na kodi | 28,118,753.1 | 28,118,753.1 | 28,777,081.1 | 2,882,765.2 | 3,108,747.8 |
| Ushuru wa forodha | 10,520,765.7 | 10,523,055.0 | 10,725,676.0 | 931,901.8 | 1,012,051.5 |
| Kodi ya bidhaa na huduma | 5,671,520.3 | 5,671,520.3 | 5,611,926.1 | 529,922.4 | 490,901.9 |
| Kodi ya mapato | 10,070,031.9 | 10,070,031.9 | 10,444,524.2 | 1,272,057.6 | 1,441,841.9 |
| Kodi nyingine | 1,856,435.2 | 1,854,145.9 | 1,994,954.8 | 148,883.3 | 163,952.5 |
| Mapato yasiyotokana na kodi | 5,135,552.7 | 5,016,314.4 | 4,631,508.3 | 561,501.9 | 470,449.5 |
| Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa | 1,356,340.7 | 1,356,340.7 | 1,438,855.3 | 127,541.0 | 174,195.6 |
| Jumla ya matumizi[1] | 41,806,195.0 | 42,152,004.4 | 41,025,758.5 | 3,169,398.9 | 3,349,998.4 |
| Matumizi ya kawaida | 27,035,891.7 | 27,288,404.6 | 26,424,396.5 | 2,215,201.3 | 2,440,572.0 |
| Mishahara | 11,767,987.1 | 11,767,987.1 | 11,238,562.9 | 997,047.1 | 970,716.1 |
| Malipo ya riba za mikopo | 5,581,973.2 | 5,643,880.1 | 5,176,700.0 | 448,472.5 | 571,279.3 |
| Ya ndani | 3,146,668.0 | 3,146,668.0 | 3,243,016.9 | 326,400.7 | 390,577.9 |
| Ya nje | 2,435,305.2 | 2,497,212.1 | 1,933,683.1 | 122,071.8 | 180,701.4 |
| Matumizi mengine ya kawaida | 9,685,931.4 | 9,876,537.5 | 10,009,133.6 | 769,681.7 | 898,576.6 |
| Matumizi ya maendeleo | 14,770,303.3 | 14,863,599.8 | 14,601,361.9 | 954,197.6 | 909,426.4 |
| Fedha za ndani | 11,129,465.2 | 11,222,761.6 | 11,999,102.9 | 756,148.1 | 672,814.1 |
| Fedha za nje | 3,640,838.1 | 3,640,838.2 | 2,602,259.0 | 198,049.5 | 236,612.2 |
| Nakisi ya bajeti bila ya misaada | -7,195,548.6 | -7,660,596.3 | -6,178,313.7 | 402,409.1 | 403,394.4 |
| Misaada | 794,390.7 | 794,390.3 | 795,481.8 | 78,659.6 | 52,966.9 |
| Ya bajeti | 109,024.4 | 109,024.1 | 52,966.9 | 0.0 | 52,966.9 |
| Ya miradi | 572,957.3 | 572,957.2 | 669,191.2 | 78,659.6 | 0.0 |
| Ya kisekta | 112,409.0 | 112,409.0 | 73,323.7 | 0.0 | 0.0 |
| Nakisi ya bajeti ikijumuisha misaada | -6,401,157.9 | -6,866,206.0 | -5,382,831.9 | 481,068.7 | 456,361.3 |
| Marekebisho (Adjustments to cash and other items (net)) | 0.0 | 0.0 | -889,834.7 | 0.0 | 84,826.7 |
| Balansi ya jumla | -6,401,157.9 | -6,866,206.0 | -6,272,666.7 | 481,068.7 | 541,188.0 |
| Ugharamiaji wa nakisi ya bajeti | 6,401,157.9 | 6,866,206.0 | 6,272,666.7 | -481,068.7 | -541,188.0 |
| Ufadhili kutoka nje halisi | 3,805,740.9 | 4,963,671.8 | 2,468,583.6 | 296,736.1 | 164,760.3 |
| Mikopo | 7,256,377.8 | 8,414,308.4 | 5,593,278.3 | 877,321.1 | 518,397.4 |
| Mikopo ya bajeti | 1,380,750.5 | 1,597,718.0 | 2,076,974.4 | 216,968.0 | 322,385.3 |
| Mikopo ya miradi | 5,875,627.3 | 6,816,590.4 | 3,516,303.9 | 660,353.1 | 196,012.1 |
| ambayo: Mikopo ya masharti ya kibiashara | 2,986,638.2 | 3,927,601.4 | 1,729,837.9 | 540,963.2 | 0.0 |
| Mikopo ya kisekta | 66,482.8 | 66,483.0 | 73,278.2 | 0.0 | 40,600.2 |
| Marejesho ya mitaji ya mikopo ya nje | -3,517,119.6 | -3,517,119.6 | -3,197,972.8 | -580,585.1 | -394,237.3 |
| Ufadhili wa ndani halisi[2] | 2,595,417.0 | 1,902,534.2 | 3,804,083.0 | -777,804.8 | -705,948.3 |
| Mikopo kutoka benki na vyanzo vingine | 2,595,417.0 | 1,902,534.2 | 3,804,083.0 | -777,804.8 | -705,948.3 |
| Mikopo ya benki | 2,300,791.1 | 1,694,165.4 | 110,423.5 | -689,510.2 | -1,430,757.2 |
| Mikopo toka vyanzo vingine (baada ya marejesho ya mitaji ya miko | 294,625.8 | 208,368.8 | 3,693,659.5 | -88,294.6 | 724,809.0 |
| Mikopo ya ndani (rollover) | 4,022,373.0 | 4,022,373.0 | 4,087,193.3 | 712,868.6 | 340,468.9 |
| Kulipa mitaji ya mikopo ya ndani | -4,022,373.0 | -4,022,373.0 | -4,087,193.3 | -712,868.6 | -340,468.9 |

Chanzo: Wizara ya Fedha

Note: [1] Haijajumuisha marejesho ya mitaji ya mikopo na matumizi yaliyochelewa (expenditure float); [2] Thamani chanya ina maana ya ufadhili, na thamani hasi ina maana ya malipo au ongezeko la amana

**Jedwali A3: Takwimu za Kifedha**

Shilingi Bilioni

| | Jul-24 | Ago-24 | Sep-24 | Okt-24 | Nov-24 | Des-24 | Jan-25 | Feb-25 | Mac-25 | Apr-25 | Mei-25 | Jun-25 | Jul-25 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Rasilimali halisi za nje | 12,226.7 | 13,100.6 | 13,704.3 | 13,773.6 | 13,296.5 | 13,558.2 | 13,242.1 | 14,706.2 | 15,442.1 | 14,658.6 | 14,028.1 | 15,509.5 | 15,726.1 |
| Rasilimali halisi za nje za Benki Kuu | 12,227.6 | 12,581.4 | 12,804.0 | 12,668.2 | 11,445.5 | 11,863.4 | 11,480.8 | 13,020.1 | 13,217.7 | 12,273.9 | 11,844.6 | 13,623.0 | 13,884.0 |
| Rasilimali halisi za nje za mabenki | -0.9 | 519.2 | 900.3 | 1,105.4 | 1,851.0 | 1,694.8 | 1,761.4 | 1,686.1 | 2,224.4 | 2,384.7 | 2,183.6 | 1,886.5 | 1,842.1 |
| Rasilimali halisi za ndani | 34,704.7 | 34,591.9 | 34,360.2 | 35,469.4 | 36,221.2 | 35,346.8 | 36,592.4 | 35,942.2 | 36,699.8 | 38,679.1 | 39,313.4 | 39,973.8 | 40,565.0 |
| Madai ya ndani | 47,250.2 | 47,176.6 | 47,160.9 | 48,136.2 | 48,998.9 | 47,559.0 | 49,255.1 | 48,836.1 | 50,109.3 | 51,989.3 | 52,813.1 | 52,610.3 | 52,147.8 |
| Madai halisi kwa Serikali Kuu | 11,895.7 | 11,445.7 | 10,986.7 | 11,618.5 | 12,257.1 | 11,461.6 | 12,679.0 | 11,853.4 | 12,110.0 | 13,233.5 | 13,021.1 | 12,061.2 | 11,175.6 |
| Mikopo kwa sekta binafsi | 35,354.6 | 35,730.9 | 36,174.1 | 36,517.8 | 36,741.8 | 36,097.4 | 36,576.1 | 36,982.7 | 37,999.3 | 38,755.8 | 39,792.0 | 40,549.0 | 40,972.2 |
| Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) | 46,931.4 | 47,692.5 | 48,064.6 | 49,243.0 | 49,517.7 | 48,905.0 | 49,834.5 | 50,648.4 | 52,141.9 | 53,337.7 | 53,341.5 | 55,483.3 | 56,291.1 |
| Fedha zilizo kwenye mzunguko | 7,085.6 | 7,302.0 | 7,353.5 | 7,408.2 | 7,597.1 | 7,351.6 | 6,997.7 | 6,954.5 | 7,190.0 | 7,024.1 | 7,438.9 | 7,874.8 | 8,122.1 |
| Amana za hundi | 21,823.8 | 21,862.2 | 22,280.0 | 22,663.5 | 22,617.6 | 22,454.7 | 23,353.0 | 23,777.1 | 24,483.7 | 25,351.5 | 25,031.6 | 25,988.2 | 26,155.5 |
| Amana za akiba na muda maalumu | 18,022.0 | 18,528.3 | 18,431.1 | 19,171.3 | 19,303.0 | 19,098.7 | 19,483.8 | 19,916.7 | 20,468.2 | 20,962.1 | 20,871.0 | 21,620.3 | 22,013.5 |
| Fedha taslim (M0) | 10,896.5 | 11,053.1 | 11,133.7 | 11,765.8 | 11,859.0 | 12,024.5 | 11,670.3 | 12,078.7 | 11,793.1 | 11,878.9 | 11,800.7 | 12,451.7 | 13,423.8 |
| Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) | 46,931.4 | 47,692.5 | 48,064.6 | 49,243.0 | 49,517.7 | 48,905.0 | 49,834.5 | 50,648.4 | 52,141.9 | 53,337.7 | 53,341.5 | 55,483.3 | 56,291.1 |
| Amana za fedha za kigeni (FCD) | 11,450.8 | 11,998.8 | 12,427.9 | 12,745.0 | 12,345.2 | 11,765.3 | 12,419.3 | 12,818.2 | 13,605.9 | 13,846.3 | 13,543.4 | 13,769.3 | 13,653.2 |
| *Amana za fedha za kigeni (Dola milioni)* | *4,323.4* | *4,470.1* | *4,575.0* | *4,753.2* | *4,708.5* | *4,954.3* | *4,995.3* | *4,951.9* | *5,120.7* | *5,169.1* | *5,045.8* | *5,286.6* | *5,369.8* |
| Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) | 35,480.6 | 35,693.7 | 35,636.6 | 36,498.0 | 37,172.5 | 37,139.7 | 37,415.2 | 37,830.2 | 38,536.0 | 39,491.4 | 39,798.1 | 41,714.0 | 42,637.9 |
| Amana za akiba na muda maalum zilizo katika shilingi ya Kitanzania | 13,304.6 | 13,607.9 | 13,811.2 | 14,224.2 | 14,355.4 | 14,234.2 | 14,342.2 | 14,711.5 | 14,994.3 | 15,478.3 | 15,583.2 | 16,060.1 | 16,406.3 |
| Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1) | 22,176.0 | 22,085.9 | 21,825.4 | 22,273.8 | 22,817.1 | 22,905.5 | 23,073.0 | 23,118.8 | 23,541.7 | 24,013.1 | 24,214.9 | 25,653.9 | 26,231.6 |
| Fedha zilizo kwenye mzunguko | 7,085.6 | 7,302.0 | 7,353.5 | 7,408.2 | 7,597.1 | 7,351.6 | 6,997.7 | 6,954.5 | 7,190.0 | 7,024.1 | 7,438.9 | 7,874.8 | 8,122.1 |
| Amana za hundi | 15,090.3 | 14,783.8 | 14,471.9 | 14,865.6 | 15,219.9 | 15,553.9 | 16,075.4 | 16,164.2 | 16,351.7 | 16,989.0 | 16,776.0 | 17,779.1 | 18,109.4 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## Jedwali A4: Mwenendo wa Riba

Asilimia

| | 2024 | | | | | | | | | | | | 2025 | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Jan | Feb | Mac | Apr | Mei | Jun | Jul | Ago | Sep | Okt | Nov | Des | Jan | Feb | Mac | Apr | Mei | Jun | Jul |
| A: Riba za mikopo/amana zilizo katika shilingi | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 1. Riba katika soko la fedha baina ya mabenki | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| Siku 1 (Overnight) | 6.75 | 6.35 | 6.20 | 6.51 | 7.02 | 6.92 | 6.80 | 7.62 | 7.88 | 7.74 | 7.73 | 7.07 | 7.69 | 7.87 | 7.91 | 7.90 | 7.95 | 7.93 | 6.62 |
| Siku 2-7 | 7.29 | 7.20 | 7.17 | 7.04 | 7.35 | 7.40 | 7.42 | 7.83 | 8.26 | 8.17 | 8.11 | 7.38 | 7.74 | 8.02 | 8.02 | 7.98 | 7.96 | 7.96 | 7.43 |
| Siku 8-14 | 7.22 | 7.21 | 7.03 | 7.25 | 7.26 | 7.42 | 7.50 | 8.29 | 8.51 | 8.81 | 8.23 | 7.68 | 8.51 | 8.62 | 8.21 | 8.08 | 8.28 | 8.12 | 7.57 |
| Siku 15-30 | 7.45 | 7.58 | 7.03 | 7.70 | 7.35 | 7.88 | 7.72 | 8.34 | 9.00 | 9.00 | 9.10 | 9.40 | 8.58 | 8.77 | 8.44 | 8.37 | 8.35 | 6.95 | 7.12 |
| Siku 31-60 | 6.28 | 7.23 | 7.85 | 7.85 | 7.88 | 7.17 | 8.18 | 9.95 | 7.56 | 9.46 | 7.88 | 8.88 | 9.03 | 8.00 | 9.83 | 8.53 | 8.53 | 8.53 | 8.53 |
| Siku 61-90 | 6.52 | 6.52 | 6.52 | 6.75 | 8.50 | 11.50 | 9.50 | 9.50 | 9.50 | 9.50 | 9.00 | 9.00 | 6.75 | 7.00 | 9.83 | 9.11 | 9.14 | 9.14 | 9.14 |
| Siku 91-180 | 9.97 | 9.29 | 8.50 | 9.73 | 9.29 | 10.35 | 6.75 | 7.00 | 9.00 | 10.96 | 7.87 | 7.87 | 7.87 | 10.42 | 10.08 | 12.00 | 12.00 | 12.00 | 11.39 |
| Zaidi ya siku 180 | 11.00 | 11.76 | 11.76 | 9.00 | 9.00 | 9.00 | 10.86 | 10.93 | 10.93 | 10.93 | 10.93 | 10.93 | 10.93 | 10.93 | 10.93 | 10.93 | 10.93 | 10.93 | 10.93 |
| Riba ya jumla | 7.27 | 7.20 | 7.10 | 7.02 | 7.34 | 7.36 | 7.24 | 7.79 | 8.16 | 8.04 | 8.06 | 7.41 | 7.80 | 8.06 | 8.12 | 8.00 | 7.98 | 7.94 | 7.35 |
| mabenki na Benki Kuu (Lombard rate) | 7.50 | 7.50 | 7.50 | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 7.75 |
| 3. Riba ya mikopo ya muda mfupi toka kwa mabenki(RE | 2.43 | 2.43 | 5.30 | 5.30 | 5.30 | 5.30 | 5.30 | 5.30 | 5.30 | 5.30 | 5.30 | 5.30 | 5.30 | 5.30 | 5.30 | 5.30 | 5.30 | 5.30 | 5.77 |
| 4. Riba ya mikopo ya muda mfupi kwa mabenki(Revers | 6.29 | 5.81 | 5.74 | 6.57 | 6.57 | 6.57 | 6.57 | 7.88 | 8.00 | 8.00 | 7.72 | 6.26 | 7.21 | 7.21 | 7.21 | 7.21 | 7.21 | 7.21 | 7.21 |
| 5. Riba ya dhamana za serikali | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| Siku 35 | 6.29 | 6.29 | 5.93 | 5.93 | 5.93 | 5.93 | 5.93 | 5.93 | 5.93 | 5.93 | 5.93 | 5.93 | 6.50 | 6.50 | 6.50 | 6.50 | 6.50 | 6.50 | 6.50 |
| Siku 91 | 8.50 | 8.43 | 8.17 | 8.07 | 8.07 | 8.07 | 5.13 | 5.13 | 5.94 | 5.94 | 5.94 | 5.94 | 7.76 | 7.76 | 7.42 | 7.50 | 7.50 | 7.50 | 7.46 |
| Siku 182 | 9.30 | 8.93 | 8.61 | 8.45 | 8.22 | 6.57 | 6.57 | 7.30 | 7.30 | 8.17 | 8.30 | 8.30 | 8.20 | 8.20 | 8.20 | 8.47 | 8.47 | 8.24 | 8.24 |
| Siku 364 | 11.81 | 12.25 | 11.82 | 10.38 | 7.83 | 6.75 | 8.84 | 10.63 | 10.98 | 11.66 | 12.78 | 12.95 | 12.63 | 11.99 | 10.11 | 8.92 | 8.92 | 8.92 | 8.13 |
| Riba ya jumla | 11.76 | 12.21 | 11.65 | 10.33 | 7.86 | 6.75 | 8.81 | 10.61 | 10.85 | 11.55 | 12.68 | 12.95 | 12.51 | 11.93 | 10.10 | 8.86 | 8.86 | 8.89 | 8.13 |
| 6. Riba za hati fungani za serikali | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| Miaka miwili | 11.64 | 11.64 | 11.64 | 11.64 | 11.64 | 11.64 | 11.64 | 11.64 | 11.64 | 11.64 | 11.64 | 11.64 | 11.64 | 12.55 | 12.55 | 12.08 | 12.08 | 12.08 | 12.17 |
| Miaka mitano | 10.09 | 10.09 | 10.09 | 10.09 | 10.09 | 10.09 | 10.09 | 10.09 | 10.09 | 12.41 | 12.41 | 12.41 | 12.41 | 12.41 | 13.14 | 13.14 | 12.94 | 12.94 | 13.18 |
| Miaka saba | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 |
| Miaka kumi | 12.03 | 12.03 | 12.03 | 12.30 | 12.30 | 12.30 | 12.30 | 13.26 | 13.26 | 13.26 | 13.26 | 13.26 | 14.08 | 14.08 | 14.08 | 14.26 | 14.26 | 14.26 | 13.74 |
| Miaka kumi na tano | 12.75 | 13.66 | 13.66 | 13.66 | 15.16 | 15.16 | 15.05 | 15.05 | 15.35 | 15.76 | 15.76 | 15.76 | 15.76 | 15.76 | 14.63 | 14.63 | 14.63 | 14.63 | 14.63 |
| Miaka ishirini | 13.51 | 15.83 | 15.51 | 15.24 | 15.24 | 15.13 | 15.17 | 15.40 | 15.45 | 15.76 | 15.64 | 15.71 | 15.71 | 15.28 | 15.28 | 15.11 | 15.11 | 14.50 | 14.50 |
| Miaka ishirini na tano | 14.39 | 14.39 | 16.79 | 16.13 | 16.13 | 15.38 | 15.38 | 15.38 | 15.42 | 15.42 | 15.93 | 15.93 | 15.84 | 15.84 | 15.84 | 15.84 | 15.29 | 14.80 | 14.80 |
| 7 Riba inayotumika kutathmini dhamana zinazorejeshwa kabla ya kuiva | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 8.50 | 8.50 | 8.50 | 8.50 | 8.50 | 8.50 | 8.50 | 8.50 | 8.50 | 8.50 | 8.50 | 8.50 | 8.50 | 8.50 | 8.50 | 8.25 |
| 8. Riba za amana za akiba | 2.69 | 2.54 | 2.70 | 2.79 | 2.87 | 2.86 | 2.87 | 3.02 | 2.84 | 2.85 | 2.69 | 2.84 | 2.97 | 2.98 | 2.86 | 2.89 | 2.52 | 2.90 | 2.90 |
| 9. Riba za jumla za amana za muda maalum | 7.40 | 7.39 | 7.55 | 7.44 | 7.65 | 7.66 | 8.15 | 7.98 | 8.20 | 8.25 | 8.18 | 8.33 | 8.31 | 8.13 | 8.00 | 7.82 | 8.58 | 8.74 | 8.83 |
| Mwezi 1 | 7.48 | 7.83 | 8.36 | 8.94 | 9.18 | 8.70 | 8.39 | 8.67 | 9.05 | 9.49 | 10.62 | 10.68 | 9.60 | 9.90 | 9.88 | 7.94 | 10.47 | 9.90 | 11.50 |
| Miezi 2 | 9.00 | 8.52 | 9.16 | 8.58 | 9.01 | 8.47 | 8.93 | 8.31 | 8.35 | 8.55 | 8.14 | 8.90 | 9.61 | 9.02 | 8.81 | 8.78 | 9.25 | 9.85 | 10.75 |
| Miezi 3 | 8.63 | 8.85 | 8.81 | 8.52 | 8.65 | 9.38 | 9.10 | 8.66 | 8.87 | 8.68 | 8.91 | 9.26 | 8.84 | 9.24 | 9.42 | 9.43 | 9.85 | 11.12 | 10.19 |
| Miezi 6 | 9.13 | 9.07 | 9.15 | 9.12 | 9.37 | 9.25 | 9.09 | 8.91 | 9.15 | 9.30 | 9.19 | 9.30 | 9.86 | 9.40 | 9.68 | 9.36 | 9.82 | 10.28 | 10.28 |
| Miezi 12 | 9.15 | 9.06 | 8.94 | 8.21 | 8.97 | 9.09 | 9.01 | 8.82 | 9.12 | 10.41 | 9.63 | 9.62 | 10.08 | 9.48 | 8.14 | 9.27 | 9.72 | 9.79 | 9.88 |
| Miezi 24 | 6.06 | 6.04 | 6.05 | 6.28 | 6.02 | 6.25 | 9.96 | 9.87 | 10.02 | 8.44 | 8.29 | 7.71 | 7.23 | 6.94 | 6.90 | 6.66 | 7.49 | 6.95 | 5.99 |
| 10. Riba za amana kwa wateja wakubwa | 9.56 | 9.52 | 9.59 | 9.33 | 9.72 | 9.86 | 9.96 | 10.12 | 9.88 | 10.27 | 10.14 | 10.39 | 11.80 | 11.40 | 10.35 | 10.52 | 10.64 | 11.21 | 10.72 |
| 11. Wastani wa riba za mikopo | 15.39 | 15.44 | 15.51 | 15.42 | 15.47 | 15.30 | 15.29 | 15.26 | 15.54 | 15.67 | 15.67 | 15.71 | 15.73 | 15.14 | 15.50 | 15.16 | 15.18 | 15.23 | 15.16 |
| Muda mfupi (Hadi mwaka 1) | 15.82 | 16.10 | 16.17 | 15.93 | 15.98 | 15.57 | 15.67 | 15.50 | 15.67 | 16.06 | 15.56 | 15.74 | 15.70 | 15.77 | 15.83 | 16.15 | 15.96 | 15.69 | 15.51 |
| Muda wa kati (Mwaka 1 hadi 2) | 15.82 | 15.71 | 15.74 | 15.77 | 15.82 | 15.69 | 15.49 | 15.50 | 15.97 | 16.25 | 16.93 | 16.79 | 16.89 | 16.06 | 16.56 | 16.33 | 16.35 | 16.49 | 16.41 |
| Muda wa kati (Miaka 2 hadi 3) | 15.92 | 15.80 | 16.05 | 15.87 | 15.88 | 15.78 | 16.06 | 16.09 | 16.26 | 16.48 | 16.36 | 16.21 | 16.35 | 15.53 | 16.44 | 15.25 | 15.24 | 15.38 | 15.22 |
| Muda mrefu (Miaka 3 hadi 5) | 15.39 | 15.51 | 15.42 | 15.44 | 15.50 | 15.37 | 15.21 | 15.14 | 15.20 | 15.06 | 15.17 | 15.24 | 15.25 | 14.09 | 14.32 | 13.88 | 14.19 | 14.35 | 14.39 |
| Muda mrefu (Zaidi ya Miaka 5) | 13.97 | 14.08 | 14.15 | 14.09 | 14.18 | 14.11 | 14.02 | 14.09 | 14.59 | 14.50 | 14.35 | 14.58 | 14.45 | 14.25 | 14.36 | 14.19 | 14.17 | 14.25 | 14.28 |
| 12. Riba za mikopo kwa wateja wakubwa | 13.44 | 13.40 | 13.46 | 13.95 | 12.69 | 12.82 | 12.78 | 12.79 | 12.92 | 12.93 | 12.77 | 12.83 | 12.80 | 13.42 | 12.94 | 12.88 | 12.99 | 12.68 | 12.56 |
| B: Fedha za kigeni | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 1. Riba za amana | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| Amana za akiba | 0.04 | 0.04 | 0.91 | 0.79 | 0.90 | 0.97 | 0.53 | 1.28 | 0.91 | 0.73 | 0.71 | 0.81 | 0.90 | 0.76 | 0.77 | 0.53 | 1.33 | 0.89 | 0.83 |
| Riba za jumla za amana za muda maalum | 3.40 | 3.73 | 3.82 | 3.77 | 3.65 | 3.91 | 3.97 | 3.73 | 3.68 | 3.85 | 3.99 | 4.20 | 4.22 | 3.66 | 2.98 | 2.94 | 3.65 | 3.60 | 3.75 |
| Mwezi 1 | 2.25 | 3.92 | 3.77 | 2.94 | 3.76 | 2.96 | 2.96 | 3.52 | 4.37 | 3.31 | 3.13 | 3.58 | 4.36 | 3.52 | 3.01 | 2.43 | 2.46 | 2.47 | 2.50 |
| Miezi 2 | 2.64 | 3.41 | 2.61 | 4.20 | 2.73 | 3.37 | 4.42 | 4.49 | 2.39 | 3.56 | 3.84 | 4.72 | 4.77 | 3.50 | 2.34 | 2.08 | 3.54 | 3.52 | 3.02 |
| Miezi 3 | 4.09 | 3.20 | 4.21 | 2.80 | 2.88 | 4.42 | 4.49 | 2.36 | 3.88 | 3.93 | 4.97 | 4.79 | 4.47 | 3.31 | 2.23 | 3.62 | 3.53 | 3.03 | 4.31 |
| Miezi 6 | 3.43 | 3.66 | 3.88 | 4.39 | 4.46 | 4.38 | 3.74 | 4.40 | 4.54 | 4.59 | 4.44 | 4.36 | 3.89 | 4.11 | 3.81 | 3.55 | 4.61 | 4.92 | 4.94 |
| 9 months | 4.58 | 4.47 | 4.64 | 4.49 | 4.40 | 4.44 | 4.26 | 3.89 | 3.21 | 3.83 | 3.57 | 3.54 | 3.62 | 3.88 | 3.50 | 3.01 | 4.10 | 4.06 | 4.00 |
| Miezi 12 | 7.72 | 8.13 | 8.17 | 8.10 | 8.19 | 7.23 | 8.34 | 8.56 | 8.44 | 8.77 | 8.53 | 8.80 | 8.83 | 8.97 | 8.93 | 8.89 | 8.81 | 8.70 | 8.82 |
| Wastani riba za mikopo ya fedha za kigeni | 7.72 | 8.13 | 8.17 | 8.10 | 8.19 | 7.23 | 8.34 | 8.56 | 8.44 | 8.77 | 8.53 | 8.80 | 8.83 | 8.97 | 8.93 | 8.89 | 8.81 | 8.70 | 8.82 |
| Muda mfupi (Hadi mwaka 1) | 9.46 | 9.11 | 9.60 | 8.74 | 8.77 | 6.58 | 9.10 | 9.55 | 9.41 | 9.50 | 9.50 | 9.44 | 9.89 | 9.93 | 9.99 | 9.97 | 9.99 | 9.93 | 9.91 |
| Muda wa kati (Mwaka 1 hadi 2) | 6.90 | 7.71 | 7.77 | 7.94 | 7.89 | 7.10 | 7.48 | 7.69 | 6.75 | 7.60 | 7.74 | 7.78 | 7.58 | 7.64 | 7.94 | 8.16 | 8.39 | 8.22 | 8.23 |
| Muda wa kati (Miaka 2 hadi 3) | 8.14 | 8.44 | 8.35 | 8.47 | 8.27 | 7.63 | 8.31 | 8.28 | 8.70 | 8.76 | 8.02 | 9.19 | 8.81 | 8.57 | 8.28 | 8.23 | 8.49 | 6.88 | 7.03 |
| Muda mrefu (Miaka 3 hadi 5) | 6.67 | 7.09 | 6.49 | 6.94 | 6.94 | 6.56 | 7.35 | 7.41 | 7.52 | 8.23 | 8.01 | 8.23 | 8.18 | 9.11 | 8.61 | 8.36 | 8.17 | 9.43 | 9.42 |
| Muda mrefu (zaidi ya miaka 5) | 7.42 | 8.29 | 8.63 | 8.40 | 9.08 | 8.26 | 9.48 | 9.86 | 9.82 | 9.76 | 9.36 | 9.34 | 9.70 | 9.62 | 9.83 | 9.70 | 9.01 | 9.06 | 9.52 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## Jedwali A5: Mizania ya Malipo ya Nje

Dola za Marekani (milioni)

| | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024p |
|---|---|---|---|---|---|
| **A. Urari wa Malipo ya Kawaida** | **-1,458.5** | **-2,374.3** | **-5,482.2** | **-2,960.6** | **-2,032.0** |
| Bidhaa: Zilizouzwa nje ya nchi (f.o.b) | 6,371.7 | 6,756.2 | 7,223.8 | 7,696.6 | 9,121.6 |
| Bidhaa asilia | 808.1 | 627.9 | 766.5 | 953.3 | 1,473.3 |
| Bidhaa zisizo asilia | 5,253.3 | 5,763.0 | 6,058.4 | 6,321.6 | 7,228.8 |
| kati ya hizo: Dhahabu | 2,957.5 | 2,737.1 | 2,835.1 | 3,058.9 | 3,419.6 |
| Bidhaa zisizo rekodiwa | 310.4 | 365.4 | 399.0 | 421.6 | 419.6 |
| Bidhaa: Zilizoagizwa kutoka nje ya nchi (f.o.b) | -7,831.7 | -10,003.4 | -14,208.7 | -13,728.9 | -14,278.9 |
| *Urari wa Biashara ya Bidhaa* | -1,460.0 | -3,247.1 | -6,984.9 | -6,032.3 | -5,157.2 |
| Huduma: Mapato | 2,183.8 | 3,117.7 | 4,762.0 | 6,231.7 | 6,899.4 |
| Usafirishaji | 1,281.7 | 1,558.1 | 1,872.0 | 2,333.4 | 2,356.6 |
| Utalii | 714.5 | 1,310.3 | 2,527.8 | 3,373.8 | 3,903.1 |
| Nyingine | 187.5 | 249.3 | 362.2 | 524.4 | 639.7 |
